epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Alhamisi Aprili 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581636

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**Samia** aagiza mambo matano Tume ya Ulinzi Taarifa Binafsi

UKURASA 2



**Mapya** yaibuliwa mabasi yaliyoungua na kuua abiria wake

UKURASA 4

**Auawa** kisha mwili kufukiwa ndani ya nyumba

UKURASA 4

**UNITED PIGO JUU YA PIGO**

UKURASA 22

# Siri ya Makalla kiti cha Makonda

UKURASA 2





Katibu Mkuu wa Umoja wa Wazazi Tanzania, Ally Hapi



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, John Mongella



Katibu Mkuu wa UVCCM, Jokate Mwegelo



Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla

TAHARIRI

## Hatukutendewa haki katika hili

KAZI ya uandishi wa habari ni pamoja na kutoa taarifa, kuelimisha na kuburudisha. Ili mwananchi apate haki yake ya kupata taarifa, jukumu la vyombo vya habari ni kukusanya na kuzisambaza kupitia vyombo vyake vikiwamo magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii kwa kuzingatia

UKURASA 6



Baadhi ya nyumba kwenye vitongoji vya Kanga, Kiegele, Kilindi na Nyandote katika kata ya Chumbi, wilayani Rufiji mkoani Pwani, zikiwa zimezingirwa na mafuriko yaliyosababishwa na kufunguliwa kwa maji kutoka Mradi wa Bwawa la uzalishaji umeme la Julius Nyerere (JNHPP). Kwa mujibu wa Mkuu wa wilaya hiyo, Meja Edward Gowele tathimini ya awali imebaini kuharibiwa kwa nyumba 58, huku hekta zaidi ya elfu 28 za mazao ya kilimo na biashara kama vile mahindi, mpunga, ufuta na ndizi zimeathiriwa. **PICHA: PROJESTUS BINAMUNGU**

## Kata 12 zafurika maji kufunguliwa Bwawa la Nyerere

UKURASA 4

# PM: Viwanda viwili vipya vinamaliza uhaba sukari

UK. 5

**MICHEZO** **WACHEZAJI YANGA WALA KIAPO SAUZI** UK.24

**KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisoma hotuba ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2024/2025, Bungeni jijini Dodoma jana. Habari Uk. 05. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia aagiza mambo 5 wizara, Tume ya Ulinzi Taarifa Binafsi

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezindua Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kutoa maelekezo matano kwa wizara na taasisi za umma, huku akitoa miezi tisa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) iwe imesomana.

Kadhalika, ameitaka Tume hiyo kuhakikisha taasisi zote za umma na binafsi zinasajiliwa na kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kabla ya mwezi Desemba, mwaka huu.

Rais Samia alitoa maagizo hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa binafsi iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

"Pili, taasisi zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi zihakikishe zinazingatia matakwa ya sheria ya ulinzi binafsi na tume itoe elimu kusisitiza wajibu wa taasisi hizo.

"Tatu, maofisa Tume mna kazi kubwa ninataka muifanye kwa weledi na ubora zaidi muwe wadhibiti, lakini pia wawezeshaji ili watoa huduma mbalimbali waridhike na utunzaji wa haki binafsi nchini.

Pia, alitaka jitihada zilizofanywa kwa muda mrefu, wizara na Tume wakazitimize.

Jambo la nne, alilielekeza kwa Waziri Nape kwa upande wa sera wafuatilie kwa karibu kazi za Tume ili malalamiko yanayoibuliwa yashughulikiwe kwa haki.

Aliiagiza wizara hiyo impelekee taarifa ya utekelezaji mara mbili kwa mwaka ili kujua mwenendo wake.

"Mkurugenzi Mkuu wa Tume na Mwenyekiti wote ni polisi, tunategemea kuona utendaji haki wa kesi na uendeshaji wake yanakwenda kama mafunzo ya kipolisi yanavyosema," alisema.

Jambo la tano, Rais Samia alilielekeza kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kusimamia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yote isomane.

Alisema kuna taasisi muhimu zipo maeneo mbalimbali, akitoa mfano, NIDA, E-Ga na Tume hiyo, akitaka ziwe na mratibu asiyefungamana na upande wowote.

Kuhusu suala la taarifa binafsi, Rais Samia alisema miaka ya nyuma duniani kuna visa vilitokea kutokana na kuvuja taarifa.

Pia, alisema vitendo vibaya vilivyofanywa na watu na vikundi visivyo vyema, kudukua mifumo ya taasisi zinazokusanya taarifa binafsi yakionesha ukiukwaji wa haki za watu.

Hayo yote alisema yalisababishwa na udhibiti hafifu wa mifumo ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa taarifa binafsi katika taasisi mbalimbali.

"Katika kukabiliana na haya yote ndio maana tupo hapa kuzindua Tume ya Ulinzi Binafsi. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka bayana kulindwa taarifa binafsi za watu au haki za binadamu.

Pia, alisema Ibara ya 16(2) ya Katiba imezitaka mamlaka za nchi kuweka utaratibu wa kisheria wa namna ya kulinda haki ya faragha na Ibara ya 12 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu mwaka 1948, inayataka mataifa kuweka utaratibu kuhakikisha mtu yeyote haingiliwi faragha yake.

Kikanda suala la ulinzi wa haki ya faragha limepewa kipaumbele katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na miongozo mbalimbali.

Alisema Umoja wa Afrika kupitia Mkataba wa Malawi wa mwaka 2014, unasisitiza ulinzi wa faragha.

"Mwaka 2015 nchi yetu iliunda sheria mbili kati ya hizi tatu, ya Makosa ya Mtandao na Miamala ya fedha. Sheria ya ulinzi binafsi tumeshafanya hivyo na leo (jana) tunazindua Tume," alisema.

Alisema kuundwa kwa sheria hiyo na uzinduzi wa Tume sio tu wametekeleza matakwa ya Katiba, bali ahadi ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kukamilisha wajibu wao wa kikanda na kimataifa na kwamba, hawana deni wameshakamilisha.

Rais Samia alisema zipo baadhi ya taarifa ambazo zinaweza kutumika kuhujumu jamii nzima na wakati mwingine kusababisha unyanyapaa na nyingine, zinaweza kuleta vurugu au vita na mauaji.

"Sasa hii haikuwa sawa. Licha ya taarifa binafsi kutumika kwa hujuma, lakini pia ni biashara kubwa kwa kampuni mbalimbali za kimtandao, hivyo hatuna budi kulindana ili zisitumike."

Alisema serikali imelazimika kuweka utaratibu wa kisera na kisheria ili kulinda taarifa binafsi za Watanzania zinazokusanywa na kuchakatwa, kuhifadhiwa na wakati mwingine kusafirishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Leo tunapozindua Tume hii, Tume itambue ina kazi nzito na ni muhimu kwa maisha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

"Usalama wetu kiuchumi, kisiasa na kijamii upo mikononi mwenu Mwenyekiti wa Tume na Mkurugenzi wa Tume na wajumbe na wafanyakazi wa Tume maisha yetu yapo mikononi mwenu, heshima zetu zipo mikononi mwenu," alisema.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema tukio la uzinduzi wa Tume limeiweka Tanzania katika orodha ya nchi za wastaarabu duniani wanaoheshimu utawala wa sheria, ubinadamu na faragha za watu na kuchangia katika jitihada za dunia kufanya ulimwengu wa mtandao kuwa salama.


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA (MARUDIO).**

Kwa Idhini tuliyopewa na **C&F Law Advocate** Kwa niaba ya **BANK OF INDIA** Tutauza kwa mnada wa hadhara (marudio) dhamana ya mdaiwa wa **BANK OF INDIA** ambayo ni nyumba ya makazi kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | **DAVID SIMON MZENA** | Nyumba ya makazi yenye Kiwanja Na 684, kitalu" B" Kinyerezi Wilaya ya Ilala CT no.94594 iliyopo kwa jina la DAVID SIMON MZENA. | 09/04/2024 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**C &F Law advocate,**
**3rd Floor Diamond Plaza,**
**Mirambo/Samora Ave,**
**P.O.BOX 70280**
**DAR ES SALAAM.**
**0659 734720**


# Siri ya Makalla

**Romana Mallya na Beatrice Shayo**

BAADA ya jina lake kuteka tetesi za waliokuwa wanatajwa kuwa na nafasi kubwa kurithi kiti cha Paul Makonda, hatimaye Amos Makalla amechaguliwa kuwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Jana, Halmashauri Kuu ya CCM ilimchagua Makalla kushika wadhifa huo sambamba na Mkuu wa Mkoa mwenzake John Mongella anayekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, akichukua nafasi ya Anamringi Macha, ambaye leo anaapishwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga.

Vilevile, uchaguzi unamhusu Ally Salum Hapi anayekuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM, akirithi kiti vha Gilbert Kalima, ambaye sasa ni Mkuu wa Wilaya ya Mkinga.

Mwingine ni aliyechipukia katika ukuu wa wilaya, Jokate Mwegelo, sasa anakuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), akihama kutoka nafasi kama hiyo katika Umoja wa Wanawake wa CCM, huku anayebadilishana naye kiti sasa, Fakii Lulandala, akihamia ukuu wa wilaya Simanjiro.

Aprili 3, mwaka huu Makonda aliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, akichukua nafasi ya Mongella.

**SIRI YA MAKALLA**

Mchambuzi wa siasa, Dk. George Kahangwa, ambaye ni Mhadhiri wa fani ya Elimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), aliiambia Nipashe jana kuwa 'mkeka' huo ulitabiriwa baada ya mabadiliko aliyofanya Rais Samia hivi karibuni.

"Mtu kama Mongella na Makalla wangerudishwa katika nafasi za kichama. Imetokea kama ilivyokuwa ikijadiliwa katika mitandao ya kijamii. Ni jambo lililotarajiwa, hawa ni watu ambao wamekuwapo katika chama.

"Mfano, Makalla amewahi kushika nafasi ya uhazini ndani ya CCM, wanaweka watu wanaokijua chama. Jokate amekuwa kwa wanawake na sasa amekwenda vijana," alisema.

Dk. Kahangwa alisema kinachoonekana kumekuwa na mabadilishano kati ya nafasi za chama na za wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya.

"Aliyekuwa katibu mkuu amekwenda kuwa mkuu wa mkoa, hii ndio picha tunayoiona. Hivyo, wakati wowote unaweza kuhamia katika nafasi hizi kama tulivyoona Hapi alikuwa mkuu wa mkoa na amerudi katika chama.

"Tunaelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu. Kwahiyo, nafasi zote hizi mbili kwenye chama na ukuu wa mkoa na wilaya au ukurugenzi wa halmashauri zinahusika moja kwa moja na uchaguzi kuhakikisha chama kinashinda na kwa nafasi za uongozi wa kisiasa wao wanahakikisha chama kinakuwa na mvuto," alisema.

Dk. Kahangwa pia alisema hizo ni timu zilizobadilisha nafasi; hakuna jipya kwa timu na wachezaji ni walewale, wanahama kwa kubadili namba tu.

Mwanaharakati wa masuala ya kisiasa na kijamii, Bubelwa Kaiza, aliiambia Nipashe jana kuwa mabadiliko yanayofanywa CCM na Mwenyekiti Samia yanatokana na kuhitaji maboresho ya kiutendaji.

Alisema baadhi ya walioteuliwa ni watu ambao walikuwa ndani ya chama, hivyo huenda Katibu Mkuu mpya, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi anaweza kuwa na mapendekezo yake kwa mwenyekiti kuhusu watu wa kufanya nao kazi kwa ufanisi majukumu ya kisiasa.

# TOVUTI MPYA

## MUONEKANO MPYA

**NIPASHE NA THE GUARDIAN KATIKA TOVUTI MOJA**

- Habari za uhakika
- Spidi katika kuperuzi
- Habari motomoto
- Michezo na makala

www.ippmedia.com



Nipashe

The Guardian www.ippmedia.com

# Mapya yaibuka mabasi yaliyoungua

## -LATRA yatoa siku saba kwa wamiliki...

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa siku saba kwa wamiliki wa mabasi ya Newforce na Sauli kutoa maelezo kwa maandishi kuhusu ajali iliyotokea hivi karibuni ikihusisha mabasi hayo pamoja na lingine lenye umiliki wa kampuni ya nchi jirani. Ajali hiyo ilitokea Machi 28, mwaka huu saa tisa alfajiri katika eneo la mashamba ya mpunga wilayani Kibaha, mkoani Pwani katika barabara ya Morogoro na kusababisha vifo vya watu viwili, majeruhi pamoja na uharibifu wa mali.

Kauli hiyo ya LATRA ilitolewa juzi baada ya kikao kilichohusisha mamlaka hiyo, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na wamiliki wa mabasi hayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, ajali hiyo ilitokana na uzembe wa dereva wa basi namba T668 DTF Scania, mali ya Mwalabhila Sauli ambalo lilitaka kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari ya watumiaji wengine wa barabara hiyo.

Ilibainishwa katika taarifa hiyo ya Jeshi la Polisi kuwa madhara ya ajali hiyo yalichangiwa na uzembe wa dereva wa basi namba T175 DZU linalomilikiwa na kampuni ya Newforce ambalo lilishindwa kuacha umbali wa gari lililokuwa mbele yake kama inavyopaswa na kusababisha vifo vya watu wawili, majeruhi na uharibifu mkubwa wa mali.

Kwa mujibu wa LATRA, kupitia mfumo wake wa kufuatilia mwenendo wa magari (VTS), tarehe ya tukio, magari hayo yalianza safari kutoka Dar es Salaam kwa pamoja saa 8:44 usiku licha ya leseni zao kuonesha kuwa yalipaswa kuanza safari saa tisa kamili na saa 10:30 alfajiri, mtawalia.

Vilevile, uchunguzi huo wa LATRA umebaini kwamba madereva wa mabasi hayo hawakutumia vitufe au batani za utambulisho wanazotakiwa kutumia wakiwa safarini. "Kwa ujumla, makosa yaliyobainika yamechangiwa na madereva pamoja na wamiliki wa mabasi husika. Mamlaka inakumbusha wamiliki na madereva kutimiza wajibu wao wa sheria katika kutoa huduma za usafiri," LATRA ilieleza katika taarifa yake hiyo iliyotiwa saini na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa mamlaka hiyo, Salum Pazzy.




Lori aina ya Howo, likiwa limeligonga gari dogo katika barabara ya Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wananchi vijiji 23 waathiriwa na mafuriko

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa vijiji 23 katika kata 12 za wilaya za Rufiji na Kibiti mkoani Pwani, wameathirika na mafuriko kutokana na kufunguliwa kwa maji katika bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere katika Mto Rufiji.

Kutokana na athari hizo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambaye pia ni Mbunge wa Rufiji, Mohamed Mchengerwa, ametoa Sh. milioni 40 kusaidia ununuzi wa mbegu kwa zaidi ya wakazi 1,000 wa maeneo mbalimbali ya wilaya ya Rufiji ambao wamekumbwa na mafurikop hayo.

Taarifa iliyotolewa na Chama cha ACT Wazalendo kupitia kwa Waziri Mkuu Kivuli, Isihaki Mchinjita, jana ilisema mafuriko hayo yameathiri vijiji 23 ambavyo ni Mloka, Mwaseni, Mtanza, Msona, Nyaminywili, Kipo, Kipugira, Ndundunyikanza, Ngorongo, Kilimani, Mkongo, Ruwe, Mgomba, Ikwiriri, Umwe, Nyamwage, Chumbi, Muhoro, Utunge, Nyandakatundu, Siasa Utete, Kipoko na King`ongo.

Kutokana na kuwapo athari hizo, chama hicho kimeiomba serikali kuwafidia wananchi hao.

"Taarifa za kutokea kwa mafuriko hayo zilianzia kutolewa Machi 12 na 14 Machi, 2024 na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliyevithibitishia vyombo vya Habari kuwa ni kweli bwawa limejaa na wameyafungilia maji ambayo yameleta na yanaendelea kuleta madhara kwa wananchi kwa kuwa zoezi ni endelevu," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia ilitaja athari zilizosababishwa hadi sasa kuwa ni pamoja na kusombwa kwa mazao, kuongezeka kwa idadi kubwa ya viboko na mamba ambao wamejeruhi na kuua watu.

"Aidha, kumekuwapo uharibifu wa makazi na miundombinu ya kijamii kama shule katika maeneo ya Muhuro, King'ongo, Kipoka na Ndutwa na kusababisha hofu kubwa ya njaa na kukosa makazi kwa mwaka huu," ilibainisha taarifa hiyo.

Mchinjita alisema ACT Wazalendo imefuatilia suala hilo kutoka kwa wananchi wa maeneo haya na kubaini kuwa licha ya serikali kukiri kuwapo kwa janga hilo, haijachukua hatua zozote za kuwanusuru wananchi wala wala kuwapo pole na badala yake inaendesha kampeni za kuwahamisha bila kuwafidia.

Kutokana na kuwapo kwa janga hilo, alisema chama hicho kinaishauri serikali kuchukua hatua kadhaa zikiwamo kufanya tathmini ya athari zilizopatiakana tangu kuanza kufungulia maji na kuwalipa fidia waathirika wote.

Nyingine ni serikali kuwatafutia maeneo mbadala wananchi kwa muda ambao shughuli zao za kiuchumi zimeathiriwa au kuonekana zinaweza kuathiriwa siku zijazo na mwendelezo wa mafuriko.

"Serikli itumie fedha za wajibu wa kampuni kwa jamii (CSR) ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 270 kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kunufaika na maji hayo katika kuzalishia na kukuza uchumi.

**WAZIRI ATOA MSAADA**

Waziri Mchengerwa, ametoa Sh. milioni 40 kwa ajili ya kusaidia ununuzi wa mbegu kwa zaidi ya wakazi 1,000 ambao mali, mashamba na makazi yao yameathiriwa na mafuriko ya maji hayo.

Akizungumza na wakazi hao mara baada ya kufanya ziara ya kukagua athari za mafuriko hayo katika maeneo mbalimbali, Waziri Mchengerwa alisema analazimika kutoa fedha hizo ili kuwatia moyo wakazi hao kurejea shambani kulima upya baada ya mazao yao kusombwa na mafuriko hayo.

"Hili ni janga letu sote mimi na nyinyi, tuliamini kwamba ujenzi wa JNHPP utakuwa mkombozi wa mafuriko ambayo yamekuwa yanatukumba mara kwa mara lakini kwa bahati mbaya bado imejitokeza. tuendelee kuwa na imani kwamba mradi ukikamilika huenda changamoto hii ikawa imetatuliwa.

" Ninafahamu fika namna wakazi wa Rufiji mlivyokuwa mmelima kwelikweli mwaka huu, ninaomba turejee shambani tulime tena vilevile kwa kiwango kikubwa. Ninamkabidhi Mkuu wa Wilaya Sh. milioni 40 kwa kuanzia kwa ajili ya kusaidia ununuzi wa mbegu ili turejee shambani tupande tena tusije kufa kwa njaa," alisema.

Halima Mbwana mkazi wa Kijiji cha Chumbi ambaye ni miongoni mwa waathirika wa mafuriko hayo, alisema hali inazidi kuwa mbaya kuanzia chakula, malazi na makazi, hivyo wanatamani kupata wasamaria wa kuwashika mkono.

# Auawa kisha mwili kufukiwa ndani ya nyumba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Kijiji cha Mwamashimba, Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga, Andrea Mayunga (77), ameuawa kisha mwili wake kufukiwa ndani ya nyumba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Janeth Magomi, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari na kwamba tukio hilo lilitokea machi 29, mwaka huu.

Alisema mtu huyo aligundulika kuwa haonekani nyumbani kwake na alitoweka katika mazingira ya kutatanisha na baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa, lilifanya ufuatiliaji na kumpata akiwa ameuawa na mwili wake kufukiwa ndani ya nyumba ya Hang Toshaga.

Kamanda Magomi alisema baada ya kufanya uchunguzi na daktari wa serikali, iligundulika kuwa Mayunga ameuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani kisha watuhumiwa kuufukia mwili wake ndani ya nyumba ili kuficha ushahidi.

"Chanzo cha tukio hili ni kulipiza kisasi cha ugomvi uliokuwapo kati ya marehemu na familia ya mtuhumiwa. Tunawashikilia watu watatu ambao ni Mussa Samweli, Njile Nkilijiwa na Masele Bubinza ambaye ni mganga wa kienyeji. Taratibu za upelelezi zikikamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani," alisema.

Magomi pia alisema mwili wa marehemu umeshakabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya mazishi.

Mauaji kama hayo yalitokea Januari Mosi, mwaka huu, Kilosa mkoani Morogoro baada ya mkazi wa kijiji cha Kimamba A, Mohamed Omar (37) kudaiwa kumuua mke wake, Beatrice Mgongolwa (31) na kumzika ndani ya nyumba waliyokuwa wakiishi.

Baada ya mwanamume huyo kufanya unyama huo, alidaiwa kuwafanyia vitendo vya ukatili watoto watatu wa huyo mama wenye umri wa miaka 11, minane na minne kwa kuwaingilia kinyume cha maumbile.

Ilidaiwa kuwa mtuhumiwa huyo baada ya kufanya tukio hilo la mauaji, alikuwa akiwafungia watoto ndani ya nyumba na kuwalazimisha kuingiliana wenyewe kwa wenyewe wakikataa anawang'oa meno kwa chuma. Pia alidaiwa alikuwa akiwasugulia pilipili machoni.

Baada ya kumzika mwanamke huyo, mtuhumiwa huyo aliendelea kuishi katika chumba hicho na kuweka mafiga juu ya kaburi hilo na kupika chakula ili kuharibu ushahidi.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka, alisema baada ya kufanya mauaji haya, alianzisha uhusiano na mwanamke mwingine na huyo akaenda kuishi katika chumba hicho alichokitumia kumfukia mkewe.

Ilibainika kuwa alifanya mauaji hayo baada ya kuanzisha tena ugomvi na mwanamke mwingine ndipo watoto wa marehemu wakawa wanamkanya mama huyo asigombane na baba yao kwa kuwa atauawa kama mama yao.

Kutokana na hali hiyo, ndipo mama huyo alipoliarifu Jeshi la Polisi kuwapo kwa mauaji hayo, ndipo alipotiwa katika mikono ya dola.

# PM: Viwanda viwili vipya vinamaliza uhaba sukari

**Na Waandishi Wetu**, DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema ujenzi wa viwanda vipya vya sukari utamaliza uhaba wa sukari nchini ifikapo 2025/26.

Aliyasema hayo jana bungeni, jijini Dodoma wakati akiwasilisha hotuba yake kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/25.

Alibainisha kuwa mahitaji ya sukari nchini kwa mwaka 2023/24 ni wastani wa tani 807,000; matumizi ya kawaida ni tani 552,000 na mahitaji kwa ajili ya matumizi ya viwandani ni tani 255,000.

Katika kipindi hicho, Majaliwa alisema uzalishaji sukari kwa ajili ya matumizi ya kawaida ulikadiriwa kufikia tani 555,000, wakati uzalishaji halisi ulikuwa tani 367,487.54 sawa na asilimia 66.2 ya lengo.

"Kutofikiwa kwa lengo la uzalishaji kulitokana na mvua za El-Nino kuanzia mwishoni mwa mwaka 2023 ambazo zilileta athari katika uzalishaji kutokana na maji kujaa kwenye mashamba ya miwa na hivyo kuathiri shughuli za uvunaji miwa na kusimama kwa uzalishaji sukari katika viwanda vya TPC, Mtibwa, Bagamoyo na Kiwanda cha K1 cha Kampuni ya Sukari Kilombero tangu mwanzoni mwa Novemba 2023.

"Hali hiyo ilisababisha upungufu wa sukari na hivyo bei ya bidhaa hiyo kupanda katika maeneo mengi nchini. Ili kukabiliana na uhaba wa sukari uliojitokeza, serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa vibali vya kuagiza tani 100,000 za sukari kutoka nje ya nchi ambapo hadi tarehe 15 Machi, 2024, jumla ya tani 32,085.50 kati ya tani 100,000 zilizoidhinishwa zimeingizwa nchini na usambazaji unaendelea," alisema.

Waziri Mkuu alisema kiwanda kipya cha Mkulazi II (Mbigiri) chenye uwezo wa kuzalisha tani 50,000 kilianza uzalishaji Desemba, 2023.

Alisema serikali inahamasisha uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda vilivyopo ili kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 460,048 mwaka 2022/23 na kufikia tani 706,000 ifikapo mwaka 2025/26.

"Miradi mipya ya Bagamoyo Sugar na Mkulazi II ambayo imeanza uzalishaji inatarajia kuzalisha jumla ya tani 85,000 ifikapo 2025/26 na hivyo kuwezesha jumla ya uzalishaji kufikia tani 756,000," alifafanua.

Waziri Mkuu pia alisema matunda ya utekelezaji miradi ya kimkakati nchini yataanza kuonekana mwishoni mwa mwaka huu kwa kuwa mingi itakuwa imekamilika kwa asilimia 100.

Alitaja miradi hiyo ni ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma (Km.1,219), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Megawati 2,115), Daraja la Kigongo - Busisi, ujenzi wa Meli ya Mv. Mwanza, uboreshaji Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

"Hadi Februari, 2024 utekelezaji miradi hiyo uko katika hatua mbalimbali muhimu za utekelezaji, huku mingine ikitarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu," alisema Majaliwa.

Alisema Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere utekelezaji wake umefikia asilimia 96.81, kazi zote katika mradi huo zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Desemba, 2024.

Alibainisha kuwa matarajio ya serikali katika mradi wa SGR ni kuanza kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji ifikapo Julai, 2024 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma.

Alisema Serikali imeendelea kutoa fedha za utekelezaji mradi huo; Sh. trilioni 10.69 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo.

Majaliwa alisema ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (Km 300) umefikia asilimia 98.84, Morogoro - Makutupora (Km 422) asilimia 96.35, Mwanza - Isaka (Km 341) asilimia 52.69, Makutupora - Tabora (Km 371) asilimia 13.86, Tabora - Isaka (Km 165) asilimia 5.38 na Tabora - Kigoma (Km 506) asilimia 1.81.

Ili kutimiza majukumu yake kwa 2024/25, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake imeomba Bunge kuidhinisha jumla ya Sh. bilioni 350.988. Kati yake, Sh. bilioni 146.394 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 204.594 ni za matumizi ya maendeleo.

Majaliwa pia aliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 181.805 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati yake, Sh. bilioni 172.124 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 9.681 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

# TRC yapokea seti ya kwanza vichwa SGR

**Na Pilly Kigome**

TANZANIA imeweka historia kwa mara ya kwanza kupokea seti ya kwanza ya vichwa viwili vya treni ya kisasa vyenye muundo wa mchongoko (EMU) vitakavyotumika kwenye reli ya kisasa (SGR).

Waziri wa Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa kila kichwa kimoja kitakuwa na uwezo wa kubeba mabehewa manane sawa na kuchukua abiria 589 kwa mabehewa yote kwa safari moja.

Alisema vichwa hivyo vimetengenezwa Korea Kusini na vina uwezo wa kutembea kwa kasi ya kilomita 160 kwa saa. Alisema wameanza kupokea vichwa viwili kwa seti moja ya awali na mpango wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) ni kupokea seti 10.

Prof. Mbarawa alisema serikali inafanya mambo makubwa kwa ajili ya taifa la Tanzania na mikakati ni kuleta seti 10 na kila mwezi italeta seti moja. Gharama ya uletaji seti hizo ni Dola za Kimarekani milioni 190.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Amina Lumuli, alisema wako tayari kutoa huduma bora na makini kwa Watanzania katika tasnia ya reli na kuongeza kuwa wameshapokea mabehewa 65 kwa ujumla wake ambayo yakiwemo ya EMU na yale mengine ambayo yalikuja awali na yameshafanyiwa majaribio vikiwimo na vichwa tisa vya umeme.

Meneja Mradi wa Ununizi wa Treni za Mwendokasi wa TRC, Kelvin Kimario, alisema treni hizo zitakuwa na uwezo wa kudhibiti mwendo kwenye hatari, mfano, ikipita kwenye maeneo ya mahandaki.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF AGRICULTURE
COTTON DEVELOPMENT TRUST FUND

## JOB OPPORTUNITY ADVERTISEMENT

Cotton Development Trust Fund (CDTF) was incorporated in Tanzania on 4th March 2008 under Trustees Incorporation Act (CAP.318 R.E. 2002) as per certificate of incorporation No. 3352. The Fund is a replacement of the Cotton Development Fund (CDF), which was established under the auspices of the Cotton Industry Act No. 2 of 2001. Formation of the Fund was in line with the wishes of the Cotton Industry Stakeholders as outlined in the Memorandum of Understanding which was signed on 21st April 2006.

Cotton Development Trust Fund is looking for the qualified, young and dynamic Tanzanians to fill in the following vacant position under contractual basis.

**1. PROCUREMENT OFFICER (01 POST)**

**Qualifications and Experience Required**

**Education requirement:**
Holder of Bachelor Degree in Materials Management, Procurement and Supplies Management, Logistics Management or equivalent qualification from a recognised Institution and must be registered by PSPTB as Graduate Procurement and Supplies Officer with working experience in related field.

**Duties and responsibilities:**
- To processes purchase or supply control of given lines of stocks;
- To assist in clearing and forwarding functions;
- To keep record and reports for all procurement activities performed
- To support in implementing the functions of Tender Board;
- To assist in processing procurement tenders as per approved Authority's policies and procedures;
- To maintain register of approved suppliers for locally supplied items and updating it accordingly;
- To maintain register of all contracts and monitors supply of ordered goods;
- To participate in planning and forecasting supplies requirements;
- To prepare quarterly reports; and
- To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**Qualitative Requirement:**
- The candidate must have good communication skills
- Fluent in English and Kiswahili
- Must be computer literate
- Self-motivated individual
- Team Player

**Duty Station: Mwanza**

**2. STORES OFFICER (01 POST)**

**Qualifications and Experience Required**

**Education requirements:**
Holder of Bachelor Degree in any of the following field; Materials Management, Logistics Management or equivalent qualification from a recognized Institution with working experience in related field.

**Duties and responsibilities:**
- To prepare bin cards and store ledger books;
- To assist in undertaking physical distribution;
- To maintain location index design;
- To carry out continuous stock checking and Annual Stock Taking;
- To assist in the preparations of quarterly reports;
- To assist in clearing and forwarding functions;
- To assist in keeping records and reports all procurement activities
- To prepare monthly stores report of all physical and card balances;
- To undertake stock review;
- To perform any other duties as may be assigned by his/her supervisor.

**Qualitative Requirement:**
- The candidate must have good communication skills
- Fluent in English and Kiswahili
- Must be computer literate
- Self-motivated individual
- Team Player

**Duty Station: Mwanza**

**GENERAL CONDITIONS:**
i) Applicants must attach an up to date passport size photo, current Curriculum Vitae (CV) having reliable contact postal address, email address and telephone number(s).
ii) Applicants must attach their detailed relevant certified copies of Academic Certificates as follows:
- Degrees and professional certificates
- Form IV and Form VI National Examination Certificates
- Birth Certificate or National Identity Card

iii) Form IV and Form VI result slips are strictly not accepted. Presentation of forged academic certificates and other information in the CV will necessitate to legal action.
iv) Applicants should indicate three reputable referees with their reliable contacts in their CV.
v) Certificates from foreign Universities should be verified by Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Accreditation Council for Technical Education (NACTE) for foreign non degree certificates.
vi) Only qualified candidates will be contacted for further processes
vii) Application closing date will be 15th April, 2024

**Mode of Application**
Application letters should be posted, e-mailed or hand delivered to the following address:

**DIRECTOR GENERAL**
**TANZANIA COTTON BOARD**
**REGIONAL DRIVE ROAD**
**P.O. BOX 61**
**MWANZA**
**E-mail: info@tcb.go.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatukutendewa haki

INATOKA UK. 1

weledi, misingi ya taaluma pamoja na mizania.

Kutokana na ukweli huo, vyombo vya habari vina dhima kubwa kuhakikisha jamii inapata taarifa sahihi na kwa wakati. Taarifa hizo kwa kiasi kikubwa ni zile zinazohusu matukio mbalimbali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi pamoja na yale yanayotendeka nje ya mipaka ya Tanzania.

Ni wazi kwamba kutokana na umuhimu wa vyombo vya habari katika jukumu la kutoa taarifa kwa jami, vimepewa nafasi ya mhimili wa nne wa dola (usio rasmi) ukiacha Serikali, Mahakama na Bunge. Ukweli na umuhimu huo unajidhihirisha pale idadi kubwa ya viongozi hutumia vyombo vya habari katika kutoa ujumbe wao ili kuufikia umma.

Mihimili yote mitatu ya dola imekuwa inatumia vyombo vya habari kutoa taarifa mbalimbali zinazoihusu, ndiyo maana hakuna shughuli ndani ya mihimili hiyo inayoweza kufanyika pasi na kuhusisha vyombo hivyo, vinginevyo kwa masuala yasiyohitaji kuwekwa wazi kwa umma.

Pia viongozi mbalimbali wa kiserikali na kidini kila mara wanapokuwa kwenye majukwaa wamekuwa wakikemea matukio yanayoendelea katika jamii yakiwamo ya watu kujichukulia sheria mkononi na hatimaye kusababisha mauaji.

Katika mahubiri na hotuba zao wamekuwa wakikemea kuporomoka kwa mmomonyoko wa maadili hali inayosababisha taifa kupitia katika kipindi kigumu kurudisha hali sawa.

Vyombo vya habari pia vinatoa msaada mkubwa katika kufichua maovu yanayotokea katika jamii na hatimaye vyombo husika kupata taarifa na kuchukua hatua. Kwa maana hiyo, ushirikiano kati ya vyombo vya habari na taasisi zingine ni mkubwa; ndiyo maana vinashirikishwa katika kazi na matukio mbalimbali ili jamii kupata taarifa, pia kuelimika na kuburudika.

Matukio ya mauaji ya watu kushambuliana hadi kupoteza uhai kutokana na migogoro ardhi, inayojitokeza mara kwa mara. Mauaji yanayotokana na sababu za wivu wa mapenzi na watoto kuuawa kwa makosa madogo kwa miaka ya hivi karibuni yanaripotiwa kwenye vyombo vya habari na maeneo mbalimbali nchini.

Jamii pia hushirikiana na vyombo vya habari inapotokea kuna tukio lolote la hatari na kazi ya vyombo hivyo ni kufuatilia kujiridhisha kama kweli limetokea, vikipata uthibitisho kutoka kwa viongozi wa eneo husika, mashuhuda na hatimaye kwa Jeshi la Polisi au Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya/Mkoa.


Taarifa za matukio ya mauaji zinazotokea nchini, huanzia kwenye maeneo husika na kazi ya waandishi wa habari ni kufuatilia na kupata ukweli na hatimaye kuthibitisha kwenye mamlaka husika.

Vyombo vya habari, ikiwamo Nipashe, mapema wiki hii, viliripoti matukio ya mauaji yaliyofanyika mwishoni mwa wiki katika maeneo tofauti nchini na kuthibitishwa na makamanda wa polisi wa maeneo hayo. Kuripoti matukio kama hayo, hakukuwa na nia yoyote mbaya ya kuleta taharuki kwenye jamii. Lengo mahsusi lilikuwa kufichua uovu usiendelee kujitokeza na pia hatua zichukuliwe ili kudhibiti hali hiyo kuendelea kutokea.

Lengo la kuripoti matukio ya mauaji ni kutoa taarifa kwa yanayojitokeza katika jamii ili kutoa msaada ukiwamo wa kisaikolojia, kuendelea kutoa elimu kwa jamii na vilevile, watu kujiepusha kujiingiza katika migogoro inayoweza kuwasababishia kupoteza maisha.

Jana, mmoja wa viongozi alishutumu gazeti hili mbele ya Rais kwamba limeripoti kuwapo matukio ya mauaji ambayo hayapo ilhali viongozi wa Jeshi la Polisi katika maeneo husika wamethibitisha kuwapo matukio hayo. Kiongozi au mtu yeyote anapovishambulia vyombo vya habari kuwa vimetoa habari za uzushi na uongo si sahihi na huko si kuvitendea haki. Ni vyema kabla ya kutoa kauli ya kuvishutumu, mantiki na kusudio la taarifa iliyotolewa vizingatiwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Bangi hizi 'Cha Arusha' inavyozidi kutengeneza sumu kwa vijana

Na Adam Fungamwango

**KUMBE** hata Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa anajua kuwa baadhi ya vijana nchini wametopea kwenye uvutaji wa bangi mpya, maarufu kama 'Cha Arusha' na 'Skanka.'

Mpaka kiongozi mkubwa kama huyo ameliongelea suala hili mbele za watu basi ujue kuna tatizo.

Mheshimiwa Majaliwa ni kiongozi wa nchi, na kiongozi yeyote moja ya mambo ambayo anahitaji ni kwamba watu wazaliane, wapate watoto wenye nguvu na afya, wawe vijana wenye nguvu kwa ajili ya kuwa nguvu kazi kwa taifa baadaye.

Taifa lolote bila kuwa na vijana wenye nguvu kwa ajili ya kuchapa kazi haliwezi kupata maendeleo.

Utapata wapi marubani, wanajeshi, viongozi wa baadaye, wataalamu, madaktari, pamoja na sekta nyingine za teknolojia?

Lakini hawa vijana tunaowategemea sasa wameingia kwenye masuala ya uraibu wa kupindukia kiasi cha kumshtua Waziri Kuu.

Akizungumza juzi kwenye Uzinduzi wa Mbio za Mwenge uliofanyika Viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika, Moshi, mkoani Kilimanjaro, pamoja na mambo mengine, Waziri Mkuu, akionekana kusikitishwa na kuwepo na aina mpya ya bangi yenye kiasi kikubwa cha ulevi, kinachofahamika kama 'Cha Arusha' na 'Skanka.'

"Ni wakati mzuri sasa hasa vijana ambao mmekuwa mkitumika na kutumia hiki 'Cha Arusha', na 'Skanka', muache ili kunusuru maisha yenu.

Vilevi hivi vitawapoteza kwenye mwelekeo na mtalifanya taifa hili likakosa Watanzania wenye afya na nguvu.

Jambo la kusikitisha ni kwamba vijana wamekuwa wakitumia na wanafahamu hiki kitu ni kibaya, na idadi kubwa ya waraibu na waathirika ni watoto na vijana wenye umri kuanzia miaka 13 hadi 24," alisema Mheshimiwa Majaliwa.

Sijajua kwanini vijana wengi wamekuwa wakipenda kutumia vilevi ambavyo vinaelezwa kuwa vina madhara.

Baadhi wanadai ni ujana, ikielekezwa vijana wana tabia ya kujaribu vitu vingi na baadaye akili zikikomaa na kujitambua wanaacha na kuwa raia wema wanapokuwa na umri wa kati.

Hata hivyo kwenye hili la 'Cha Arusha' na 'Skanka', inaonekana watakapokuja kuwa na umri wa kati ambao wanatakiwa kuacha ujana, watakuwa tayari na shida ya afya ya akili.

Mpaka watakapofika hapo hawatokuwa na uwezo wa kuwa na familia, na watakuwa tegemezi kwa wazazi wao.

Kijana anapokuwa tegemezi kwa mzazi wake, hana uwezo wowote wa kufanya kazi, na si mlemavu, ila tu akili yake si nzuri kwa sababu ya kuvuta bangi, ni hasara kubwa si kwa mzazi, bali hata kwa taifa.

Waziri Mkuu akaenda mbali na kuitaja mikoa inayolima kwa wingi zao hilo ambalo limekuwa sumu kwa vijana wetu kuwa ni Mara, Morogoro, Arusha, Pwani na Mwanza, akamalizia kwa kutoa onyo kwa 'wakulima' hao kuacha mara moja, na akaahidi hatua kali zitachukuliwa kwa wanaojihusisha na kilimo hicho haramu.

Wakati serikali ikichukua upande wake, 'kudili' na walima sumu hao, taasisi na jamii nayo ijikite kutoa elimu kwa vijana kuachana na mambo hayo kwani naamini ikiwa wenyewe watashiba elimu hiyo, wanaolima watakosa soko.

Jamaa hao wameamua kulima kwa sababu wateja wapo kwa wingi, hivyo elimu kutoka kwa taasisi za kiafya, jamii ikiwemo wazazi wenyewe kukaa na watoto na vijana wao kuwaambia juu ya athari za kufanya hivyo.

Wazazi pia, wanatakiwa kuwafundisha watoto na vijana wao juu ya kujitegemea wakiwa bado wadogo, kuwadekeza kupita kiasi ili waweze kujitegemea wenyewe wanapokuwa vijana, kufilishika au kufariki.

Baadhi ya watoto na vijana wanajiingiza huko baada ya kuona maisha yamekuwa magumu, tofauti na ya zamani waliyokuwa wakiyapata kwa wazazi wao, hivyo kuingia kwenye uraibu hiyo, wakiona ndiyo njia ya kuondoa mawazo.

Wote tushirikiane kuiondoa sumu hii mpya ya 'Cha Arusha' na 'Skanka.'

HABARI KITAIFA



Diwani wa Kata ya Majimoto, wilayani Serengeti mkoani Mara, Johannes Masirori akizungumza na wakazi wa kata hiyo juzi, katika mkutano wa hadhara iliohusu changamoto zinazowakabili hasa suala la kuzuiwa kuchimba madini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilomita 13.5 za barabara zatengenezwa Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

BARABARA zenye urefu wa kilomita 13.5 zimekarabatiwa na Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA), wilayani Muheza.

Msimamizi wa ujenzi wa barabara hizo kutoka TARURA, Mhandisi Lidya Msumari, alisema ujenzi umeanza katika barabara Wilaya ya Muheza kwa kiwango bora ikiwamo ujenzi wa daraja katika eneo la Kwamtiga, Kata ya Genge ambalo limekamilika na litafunguliwa na Mwenge wa Uhuru Aprili 15.

Alizitaja barabara zenye urefu wa kilomita 13.5 ambazo zimekarabatiwa ni kutoka TRM-Kwemuyu, Genge-Mang'enya, Muheza High School - Kivindo, Misozwe-Kwatango, Shidepha-Kididima, Mkumbi-Muheza Estate na Mdote - Tanesco zenye bajeti ya Sh. 345,068,500.

Katika hatua nyingine Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA) wilayani Muheza, imepanga kutumia Sh. 2,420,420,000.00 kufanya matengenezo mtandao wake wa barabara.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Muheza, Mhandisi John Kwagilwa, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Alisema kuwa mpango huo wa bajeti umezingatia vipaumbele vilivyotolewa na kata husika kwa kushirikiana na viongozi madiwani na mbunge.

Alisema wananchi wote wanatakiwa kutunza barabara zote ili ziweze kutumika kwa muda mrefu.

# Mfanyabiashara adai kutaka kubambikiwa kesi ya ugaidi

**Na Kulwa Mzee**

MFANYABIASHARA wa kusindika mazao, Bertha Mabula amesema anahofia usalama wake kwa madai ya kubaini Polisi Mjini Kahama wanataka kumbambikia kesi ya ugaidi wakidai alitaka kulipua Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga wakati akifuatilia mwenendo wa shauri lake kwa ajili ya kukata rufani.

Akizungumzia tukio hilo jana, Bertha alidai alifika Mahakama Kuu kwa ajili ya kuchukua mwenendo wa shauri la madai dhidi ya mfanyabiashara Tumsime Tibaijuka ili akakate rufani kwa kutoridhishwa na uamuzi wa mahakama hiyo.

Shauri hilo la madai lilitupiliwa mbali mbele ya Jaji Frank Mahimbali, kwa mdai kudai Sh. milioni 295 alizomkopesha Tumsime pamoja na gharama zingine za usumbufu jumla kuwa Sh. bilioni 1.6.

Akisimulia tukio la madai ya kutaka kubambikiwa kesi ya ugaidi, baada ya hukumu kutolewa Machi 8, mwaka huu alirudi tena mahakamani Machi 21, mwaka huu kwa ajili ya kuchukua mwenendo wa shauri hilo.

"Wakati naenda mahakamani Shinyanga nilikodi teksi inayoendeshwa na Beatus Mandali, alinifikisha akanisubiri nilipomaliza kupata huduma tuligeuza kurudi Kahama, nilipata taarifa kuna Polisi walikuwa wananisubiri maeneo ya Tinde wanikamate, lakini kwa bahati ilinyesha mvua kubwa, wakati tunapita eneo hilo hawakutuona.

"Siku ya pili nilipata taarifa dereva Beatus alikamatwa na askari akiwa katika kituo chake cha kazi, akapelekwa Kituo cha Polisi Kahama akituhumiwa kubeba gaidi anayetaka kulipua mahakama," alidai Bertha.

Alidai dereva alipofikishwa kituoni alihojiwa kisha akaachiwa na kuambiwa asimjulishe kuhusu tukio hilo, lakini dereva aliamua kumsimulia Bertha kuwa anatafutwa kwa tuhuma za ugaidi.

"Derava aliponiambia nilimpigia simu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi kumfahamisha njama hizo na akaahidi atafuatilia tukio hilo.

"Niliendelea kuwasiliana naye kwa njia ya WhatsApp na meseji zote ninazo nikimfahamisha hofu yangu ya kubambikiwa kesi hiyo, akasema angekuja Kahama, lakini bado nasubiri huenda atakuja," alidai Bertha.

Dereva teksi, Beatus akithibitisha tukio la kukamatwa kwake kwa njia ya simu, alidai alikamatwa akiwa stendi anapofanyia kazi, askari walikwenda na karandinga la polisi kumkamata.

"Askari waliniambia wananikamata kwa sababu jana nilibeba magaidi walikuwa wamevaa hijabu, nilijibu niliyembeba kumpeleka Shinyanga mahakamani alikuwa kavaa dera.

"Walinikamata kwa kuwa nilikuwa na gari niliendesha gari yangu kuelekea Kituo cha Polisi Kahama huku nyuma nikisindikizwa na karandinga la Polisi.

"Nilihojiwa nikiwa katika ofisi ya upelelezi, niliulizwa jana nilienda wapi, nilijibu Shinyanga, nikaambiwa nilibeba magaidi wamevaa hijabu, nilijibu niliyembeba alikuwa kavaa dera, askari aliandika maelezo kwenye simu kubwa, mwingine alikuwa kabeba bunduki ndiye aliyekuwa ananipiga picha.

"Maelezo yalitumwa sikujua yalitumwa wapi, baada ya kumaliza mpelelezi, Edes Jackson aliniambia nisiende kumwambia mtu yeyote, lakini dada Bertha aliponipigia nilimwambia," alidai.

Alidai baada kumwambia Bertha alipigiwa simu na Afande Edes akamwambia alidhani ana bichwa kubwa anazo akili kumbe hana akili.

"Niliwindwa tangu mchana sikuwapo mjini, nilipoingia wakaja kunikamata, waliniambia walinivizia Tinde jana, lakini walishangaa nilipitaje hawakuniona.

"Nilikamatwa mbele ya watu wengi kituoni na waliponifuatilia kunitoa walijibiwa niko Polisi kwa ajili ya uchunguzi," alidai.

Askari mmoja anayetuhumiwa kuwapo katika msafara wa kumkamata dereva huyo alipopigiwa simu kuulizwa kuhusu tukio hilo, Afande Edes Jackson, alidai haruhusiwi kutoa taarifa yoyote kwa sababu sio msemaji.

"Unaniulizaje maswali hayo, sina mamlaka ya kutoa taarifa, muulize RPC Shinyanga, unakuja kwangu mwenye renki ndogo hivi, kwa akili ya utu uzima uliyonayo kwani mtu kukamatwa lazima aingizwe mahabusu.

"Unaweza kutuhumiwa ukakamatwa, ukapekuliwa na kuachiwa, hizo taarifa kaulize mkoani watakujibu alikamatwa, alikaa mahabusu muda gani msiniulize mimi," alidai Afande Edes akimjibu mwandishi kwenye simu.

Mfanyabiashara Tumsime anayetuhumiwa wakati dereva anakamatwa askari alimpigia simu kuuza shauri lilikuwa namba ngapi, alipoulizwa kwa kupigiwa simu kuhusu hoja hiyo alidai anamfahamu Bertha Mabula na walikuwa na kesi ambayo imeshatolewa uamuzi.

"Masuala kwamba nawafahamu askari waliomkamata dereva, mimi siwajui na kama alikamatwa kituoni kutakuwa na taarifa zake, huyo dereva wake pia simjui," alidai Tumsime.

Akizungumzia tukio hilo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Magomi alidai hana taarifa za Bertha kutaka kukamatwa kwa tuhuma za ugaidi.

"Taarifa za huyo mfanyabiashara kutaka kukamatwa mimi sina na bahati nzuri huwa nina tabia ya kukagua vitabu, Bertha Mabula, wala simjui.

"Kama anasema tuliwasiliana kwa simu labda nilisahau kama binadamu, sikumbuki, unajua kufanya kazi kwa simu mtu kama binadamu unaweza kusahau, mimi nipo aje kuniona," alidai RPC Magomi.

Baada ya shauri la madai kutupiliwa mbali, Bertha amewasilisha kusudio la kukata rufani akipinga hukumu ya Mahakama Kuu Shinyanga kwa madai kwamba hakutendewa haki na ushahidi wake wa maandishi pamoja na mashahidi wengine watano wa upande wake haukuzingatiwa.

Pamoja na kufanya hivyo pia Machi 28, mwaka huu alimwandikia barua Jaji Kiongozi yenye kichwa cha habari kutoridhishwa na uamuzi uliotolewa na Jaji Frank Mahimbali, kwenye shauri namba 03/2023.

Katika shauri hilo, mdai Bertha Mabula dhidi ya Tumsime Tibaijuka na Tunel Incorporation Limited, anadai Sh. milioni 295 alizomkopesha Tumsime kwa ajili ya kufanya biashara, ambazo anadai hajawahi kuzilipa.

KABWELA — Na Fadhili Mohammed





Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Hashil Abdallah (wapili kulia), akimsikiliza mmoja wa viongozi wa kiwanda cha kuzalisha maji tiba cha Kairuki Pharmaceutical Industry Ltd, alipofanya ziara ya kikazi pamoja na makatibu wakuu wengine kiwandani hapo, wilayani Kibaha, mkoani Pwani jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania yaanza kuuza majitiba nje ya nchi

**Na Joseph Mwendapole**

KIWANDA cha kutengeneza dawa cha Kairuki Pharmaceutical Industry Limited Kibaha mkoani Pwani, kimeanza kuuza majitiba mataifa mbalimbali Afrika.

Hayo yalisemwa jana mkoani hapa na Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda hicho, Dk. Muganyizi Kairuki, wakati wa ziara ya makatibu wakuu watatu waliokitembelea kuangalia shughuli za uzalishaji.

Makatibu wakuu hao ni kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, Wizara ya Afya, Dk. John Jingu na Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani, Rashid Mchatta.

Dk. Muganyizi alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha chupa za maji tiba milioni 50 kwa mwaka na asilimia 60 huuzwa nchini wakati asilimia 40 huuzwa nchi za nje zikiwamo Rwanda, Comorro, Malawi, Zambia, Namibia, Congo, Mozambique na Yemen

Dk. Muganyizi alitaja baadhi ya dawa zilizosajiliwa kuzalishwa kiwandani hapo kuwa ni pamoja na "Sodium Chloride (0.9%w/v), Compound Ringer Lactate, Dextrose (5%w/v) &Sodium Chloride(0.9%w/v), Dextrose (5%w/v) na Dextrose(10%w/v).

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Abdallah, alisema serikali inapongeza kiwanda hicho na kuahidi itaendelea kuwalea wawekezaji wa ndani.

Dk. Abdallah alisema lengo la ziara hiyo lilikuwa kujionea shughuli za uzalishaji, kusikiliza changamoto zinazokikabili kiwanda hicho na kutafuta suluhisho.

Aidha, alisema ziara hiyo inaonyesha dhamira ya serikali kuimarisha sekta ya viwanda nchini kwa kuwaunga mkono wawekezaji wa ndani na kuwawezesha kuchangia kikamilifu maendeleo ya uchumi wa taifa.

Dk. Abdallah alipongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa utendaji kazi mzuri na kuahidi ushirikiano kutoka kwa wizara husika kutatua changamoto zilizopo ili kuwezesha kiwanda hicho kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Vilevile, alibainisha kuwa kiwanda hicho kinachotoa ajira za moja kwa moja 200 na zisizo za moja kwa moja 300 ni moja ya kiwanda cha kimkakati kinachozalisha dawa za majitiba (Fluid Therapy) mbalimbali nchini ili kupunguza utegemezi wa kuagiza dawa hizo nje ya nchi.

## Spika aielekeza serikali ukarabati shule kongwe

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ameielekeza serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuwa na mpango maalum wa kukarabati shule kongwe za sekondari na msingi nchini ili kuziweka zote katika mazingira yanayofanana.

Dk. Tulia alitoa maelekezo hayo jana bungeni baada ya swali la Mbunge wa Mbarali (CCM), Bahati Ndingo, aliyetaka kujua ni lini serikali itakarabati shule kongwe za msingi zilizopo Mbarali na zipo katika hali mbaya.

Spika Tulia alisema, Rais Samia Suluhu Hassan, amejenga shule mpya ni muhimu zifanane na za zamani.

"Tatizo hilo lipo maeneo mengi na shule zinazoitwa kongwe nyingine sio kongwe sana wala madarasa yake sio kongwe sema wanaotumia ni watoto madarasa yanaharibika mapema, hivyo kuwe na mpango maalum wa kukarabati shule hizi ili kuzifanya zifanane," alisema.

Awali, akijibu swali la Mbunge Ndingo, alisema serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu ikiwamo ujenzi wa madarasa mapya na kukarabati chakavu. "Katika mwaka wa fedha 2022/23 na 2023/24, serikali imetumia Sh. milioni 360 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madarasa 18 mapya katika shule kongwe za Chimala, Igalako, Ujewa na Isitu," alisema.

Alisema kwa mwaka 2024/25, serikali imetenga Sh. milioni 180 kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za Ipwani, Ibumila, Mbuyuni na kusisitiza kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe kote nchini.

# Mvua yasababisha hekari 15,000 za mpunga kuzama

**Na Guriani Adolf,**
SUMBAWANGA

ZAIDI ya hekari 15,000 za mpunga zimezama kwenye maji baada ya Ziwa Rukwa kufurika na kuingia kwenye mashamba ya wakulima katika Kata ya Milepa, wilayani Sumbawanga.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wa habari hizi, wakulima hao walisema mazao yao yote yamezama kwenye maji na kuharibika huku matarajio ya kupata mavuno katika msimu huu wa kilimo yakitoweka.

Mmoja wa wakulima hao, Emmanuel Kakwaya, alisema mvua kubwa inayoendelea kunyesha mkoani humo imesababisha maji mengi kuelekea ziwani na kujaa hadi ziwa kufurika na kuingia kwenye mashamba yao kuharibu mazao.

"Pamoja na kuwa mpunga ni zao linalohitaji maji mengi, lakini haya yamezidi kiasi kwamba mpunga wote umezama kabisa ni maumivu tu kwa wakulima kwani tulitumia gharama kubwa katika kilimo na matokeo yake imekua kama hivi... mitaji yote ya kilimo imepotelea kwenye maji," alisema.

Monica Kisantola mkulima wa mpunga wa Kijiji cha Kisa, alisema baadhi ya wakulima huwa wanakopa fedha za kilimo kwa watu binafsi na taasisi za fedha na kuweka dhamana mali zao, baadhi zitauzwa na kujikuta wanashindwa kupiga hatua kutokana na hali ilivyo.

Aliiomba serikali iwasaidie kuongea na taasisi za fedha walizokopa wakulima hao ili iwaongezee muda wa marejesho ya mikopo hiyo kwa kuwa baadhi yao hawawezi kurejesha kwa wakati kwakuwa mazao waliyotegemea yameharibika na maji yaliyojaa ziwani.

Diwani wa ya Kata Milepa, Apolinary Macheta, alisema pia familia zipatazo 13,700 zimelazimika kuyakimbia makazi yao baada ya nyumba zao kuzingirwa na maji baada ya Ziwa Rukwa kufurika na kufika kwenye makazi ya watu.

Alisema mvua inayoendelea kunyesha katika Mkoa wa Rukwa inasababisha maji mengi kuelekea Ziwa Rukwa na kujaa huku miundombinu ya barabara ikisombwa huku watu watatu wakipoteza maisha kwa kufa maji wakati wakijaribu kuvuka mito iliyojaa.

Diwani huyo alisema kutokana na hali inavyoendelea kuna hofu vijiji vyote katika kata hiyo vikazama kwenye maji kwakuwa vipo pembeni ya ziwa na maji yanaendelea kujaa huku nyumba nyingi zikiendelea kuzungukwa na maji na wakazi wake wakilazimika kuzihama nyumba hizo ili kuokoa maisha na mali zao.



# Wananchi watoa angalizo vifo vitokanavyo na uzazi

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

BAADHI ya wananchi mkoani Manyara wamesema licha ya kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi, kuna haja serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuokoa kinamama na watoto wachanga.

Kwa nyakati jana, wananchi walitoa rai hiyo walipozungumza na Nipashe kuhusu vifo vitokanavyo na uzazi nchini.

Mkazi wa Kijiji cha Managha, Rehema Samweli alisema vifo hivyo vimepungua katika maeneo yao kutokana na jitihada za serikali kuongeza vituo vya afya, zahanati na hospitali ambazo zina watoa huduma.

"Ili tuendelee kupunguza vifo, ni vizuri kutoa elimu kwa wauguzi ili wawe rafiki kwa wajawazito wanapokwenda kujifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya," alishauri Samweli.

Mkazi wa Kijiji cha Mandi, Lucas Andrew alisema kuwapo vyombo vya usafiri wa uhakika kwa baadhi ya vijiji ni chanzo cha kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi.

Alisema kuwa miaka ya nyuma kuna baadhi ya maeneo yalikuwa hayapitiki ndio maana wajawazito wakawa wanapoteza maisha kwa kuwa walifikishwa hospitalini kwa kuchelewa.

Mratibu wa Uzazi, Mama na Mtoto Mkoa wa Manyara, Emma Ngatoluwa alisema vifo vya wajawazito vimepungua kutoka 49 mwaka 2022 hadi 34 mwaka jana.

Ngatoluwa alisema vifo hivyo vinapungua kutokana na elimu inayotolewa kliniki kwa wajawazito na hamasa ya kuwasisitiza wanawake kujifungulia zahanati, vituo vya afya au hospitalini.

Machi 21, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Gadabagara, alimwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Dk. Hosea Madama kuhakikisha wanatoa elimu ya mfumo wa M-Mama ambao unamwezesha mjamzito kufikishwa kituo cha afya au hospitalini mapema ili kupata huduma stahiki.

Queeb alisema mfumo huo una utaratibu wa magari yaliyoandaliwa kufuata wajawazito waliko wakipiga simu na kuwapeleka hospitalini bila malipo.

Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 nchini (TDHS-MIS 2022), kiwango cha vifo vya uzazi ni kati ya vifo 59 hadi 149 kwa kila vizazi hai 100,000.

Vilevile, kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) 2021/22-2025/26, licha ya juhudi hizo za kuokoa uhai wa mama na mtoto, vifo vitokanavyo na uzazi bado viko juu.



Diwani wa kata ya Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Salome Mnyawi (katikati), akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule ya msingi Songambele, juzi.
**PICHA: GIFT THADEY**

# Wanafunzi 1,000 wapewa miche ya miti kukabiliana na hewa ukaa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

ZAIDI ya wanafunzi 1,000 wa Shule ya Msingi Oldonyowas na Sekondari ya Oldonyowas wamepewa miche ya miti kwa ajili ya kivuli na matunda na Shirika la Compassion International ili kuhakikisha mazingira yanalindwa na kuhifadhi hewa ukaa.

Miti hiyo imetolewa kupitia huduma ya vituo ya Mtoto na Kijana, vinavyojumuisha vituo saba vya TAG, kwa lengo la kuimarisha mazingira yao.

Akizingumzia ugawaji na upandaji miti katika shule hizo, Mwenyekiti wa Claster ya Olmotonyi, Mchungaji Zakayo Sanare alisema kuna haja kuhakikisha mazingira yanalindwa na kuhifadhiwa kwa kupanda miti.

"Ili mazingira yalindwe na kutunzwa, tumeamua kugawa miti hii na kusimamia zoezi la upandaji wake, lakini pia tumetoa elimu kwa walimu dhidi ya watoto ili wanapopata changamoto za unyanyasaji kwa watoto zitatuliwe haraka," alisema.

Alisema wanaamini watoto hao wanaposhiriki katika upandaji miti, wanajenga utamaduni huo wa kuhakikisha hata maeneo yao wanayoishi yanapandwa miti kwa kuwa ndio njia sahihi ya kuhifadhi mazingira na kuyalinda. Ofisa Malezi kutoka Compassion, Evenlite Jackson alisema ni lazima watoto walindwe, ili kuwaepusha na ukatili wa kijinsia, ikiwamo unyanyasaji ili wawe na furaha nyakati zote, wakiwa shuleni na nyumbani.

"Mkiona mnapata manyanyaso hakikisheni mnaripoti sehemu husika ili hatua zichukuliwe ndani ya muda mwafaka," alisema. Mkuu wa Shule ya Msingi Oldonyowas, Filbert Macha alishukuru miti hiyo kupandwa shuleni huko, mazingira yatapendeza na wanafunzi watapata kivuli na matunda ambayo yatawasaidia kuwa na afya njema.

Aliomba wadau wengine wa elimu kutembelea kwenye shule mbalimbali kutoa elimu, ili wanafunzi wapate maarifa yatakayowasaidia kupata uelewa ikiwamo mbinu za kimaisha.

Vituo saba vya huduma ya mtoto na kijana vya TAG vinajumuisha pia Oldonyosambu, FPCT Oldonyowas, KKKT Lolmotonyi, Baptist Olmotonyi, Baptist Engokidong'oi.

# Polisi wapokea mbwa wa kunasa nyara za serikali na wahalifu

**Na Allan Isack,** BABATI

JESHI la Polisi katika mpango kazi wa kuimarisha ulinzi na usalama, limepokea mbwa watatu watakaosaidia kufanya doria na kunusa ili kukamata nyara za serikali na wahalifu.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Mbwa na Farasi Makao Makuu ya Polisi Tanzania, Mrakibu wa Polisi (SP) John Kyariga, alibainisha hayo jana wakati akikabidhi mbwa watatu mjini Babati kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, George Katabazi.

Mkuu huyo wa kikosi cha mbwa na farasi amekabidhi mbwa wa polisi watatu kwa Kamanda Katabazi ikiwa ni sehemu ya mikakati yao ya kuanzisha na kuimarisha kikosi cha mbwa na farasi mkoani mkoani Manyara.

Akizungumza baada ya kupokea mbwa hao, Kamanda Katabazi alishukuru uongozi wa polisi makao makuu na kikosi cha mbwa na farasi kwa kuwapatia mbwa hao.

"Tunashukuru kwa kuona umuhimu wa Mkoa wa Manyara, kuanzisha na kuimarisha kikosi hiki, pia kutupatia mbwa hawa watatu watakaotusaidia kupambana na uhalifu," alisema Kamanda Katabazi.

Alisema mbwa hao watakuwa na mchango mkubwa katika kusaidia askari kuimarisha doria na misako ya wahalifu.

"Mbwa hawa watatumika kunusa na kukamata watuhumiwa hususani na nyara za serikali na kufanya msako wa wahalifu kwa njia ya kunusa," alisema Kamanda Katabazi.

Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi Mkoa wa Manyara, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Edward Shija, alisema kwa sasa wako kwenye maandalizi kwa ajili ya uzinduzi rasmi wa kikosi hicho.

"Hivi karibuni, baada ya kumalizika kwa mafunzo maalum ya mbwa na farasi yanayoendelea, tutafanya uzinduzi katika kuhakikisha tunashiriki kukomesha uhalifu," alisema Shija.

Mkazi wa Mtaa wa Nyunguu mjini Babati, Renada Gwasima, alisema hatua hiyo ni maendeleo makubwa kwa askari polisi wa Mkoa wa Manyara.

Alisema wameona baadhi ya mikoa mingine nchini ikitumia mbwa na farasi katika kupambana na uhalifu, hivyo ni hatua kubwa kwa Manyara.





# Wakazi wa Gambosi walia kukosa umeme

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

WAKAZI wa Kata ya Gambosi, Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu wameomba kufikishiwa huduma ya umeme katika makazi yao ili watumie nishati hiyo kujiongezea kipato na kuchangia ukuaji uchumi nchini.

Waliwasilisha kilio chao hicho jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Simoni Simalenga, aliyezuru huko kwa lengo la kusikiliza kero mbalimbali za wananchi wa kata hiyo.

Mmoja wa wakazi wa kata hiyo, Kezia Mashyenene alisema wamekuwa wanaomba huduma hiyo kwa miaka mitatu sasa lakini hakuna hatua zilizochukuliwa kufikisha nishati hiyo katika kata yao.

"Sisi tumeomba umeme tangu mwaka juzi lakini hatuletewi umeme mpaka leo, na ni haki yetu kulisema hili kwa sababu tunashindwa kufanya kazi za kuleta maendeleo hususani zinazotegemea umeme. hivyo tunaomba mkuu wa wilaya utusaidie katika jambo hili," alisema Kezia.

Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Bariadi, Majaliwa Richard, alisema tayari wamepita katika vitongoji vyote kuainisha mahitaji ya wateja ili wapeleke miundombinu ya umeme.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24 ambao zimebaki siku 87 ufike ukomo, Kitongi cha Mwanshela, Kata ya Gambosi kitanufaika na mradi ambao tayari wameshaanzisha na wako kwenye hatua ya ukaguzi.

Kwa vitongoji vingime ambavyo havijapata umeme, Richard alisema wanaandaa utaratibu wa kupeleka umeme katika makazi ya wananchi.

"Tatizo lililopo ni kupeleka umeme kwenye vitongoji, umeme unaweza ukawa umefika senta (makao makuu ya kijiji), lakini maeneo yanayozunguka senta umeme usifike.

"Hivyo kutokana na hali hiyo Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na TANESCO tulipita katika vitongoji vyote kuanisha mahitaji ili kupeleka umeme katika vitongoji ambavyo havijapata umeme na tunapanga kulingana na bajeti inayopatikana," alisema Majaliwa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Simalenga, aliagiza TANESCO Wilaya ya Bariadi kulipatia ufumbuzi tatizo hilo na kusema iwapo kuna wananchi ambao walipeleka maombi ya kufungiwa umeme katika ofisi zao wafuatilie ili kujua kama shida ni mita za umeme au kuna tatizo tofauti na hilo.

Pia alitoa namba zake za simu kwa wananchi ili wawe na mawasiliano katika kufuatilia kwa ukaribu zaidi utatuzi wa kero hiyo ya muda mrefu.

# Wachimba mtaro kuzuia vifo mgodini

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

UCHIMBAJI mtaro kuzunguka mgodi mdogo wa Mwakitolyo, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, umeanza rasmi ili kuzuia maji ya mvua kuingia kwenye machimbo na kutitia.

Uchimbaji huo unatekelezwa na wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu mara baada ya kupokea agizo kutoka kwa Waziri wa Madini, Antony Mavunde.

Hatua hiyo inatajwa itasaidia kuokoa zaidi ya machimbo 110, maarufu maduara) yaliyokuwa kwenye hatari ya kutitia na kunusuru ukosefu wa ajira nyingi za wachimbaji hao.

Kaimu Meneja wa mgodi huo, Matemla Michael alisema eneo hilo linakadiriwa kuwa na wachimbaji 20,000 wakiwamo wajasirimali wadogo, ambao wamelazimika kutumia Sh. milioni 11.88 kuboresha machimbo yao ili kuepusha madhara, hasa vifo kwa wachimbaji.

"Tumechimba mtaro mkubwa wa kupitisha maji, tumeokoa zaidi ya maduara 110 ambayo yangetitia na kusababisha ajali na maafa kwa wachimbaji wetu, lengo letu ni kuhakikisha wanakuwa salama na kunufaika na rasilimali hiyo pasipo tatizo," alisema.

Katibu wa Mgodi huo, Leonard Waziri alisema wamefanikiwa kununua gari la kubeba wagonjwa lenye thamani ya Sh. milioni 60 na kuikabidhi serikali, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha mazingira ya upatikanaji huduma za afya.

Akizungumza kwa niaba ya wachimbaji wanawake, Janeth Ngangura, alishukuru wananchi kupewa kipaumbele katika uchimbaji madini na kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao.

Alisema kuwa awali walikuwa wanaonekana kama mkosi wa kukimbiza dhahabu, lakini baada ya elimu kutolewa kwa wachimbaji, sasa wanawake nao wananufaika na rasilimali hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro (kushoto), akizungumza na wananchi wa Old Shinyanga kwenye Mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi juzi, ambapo miongoni mwa kero zilizotawala ni migogoro ya ardhi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ukosefu taulo za kike wachochea utoro

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

UKOSEFU wa taulo za kike umetajwa kuwa chanzo cha utoro kwa wasichana katika Shule ya Sekondari Kayenze, wilayani Ilemela, mkoani Mwanza.

Shule hiyo ina wanafunzi 1,036. Kati yao, wasichana ni 538. Imepewa msaada wa taulo za kike 408 ili kuwanusuru na utoro ambao umetajwa kuwa chanzo cha kutokuzingatia masomo na kukatisha ndoto zao.

Baada ya kupokea msaada huo uliotolewa na mwandishi wa habari, Grace Mbise, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Deogratius Paulo alisema ukosefu wa taulo za kike ni kikwazo kwa watoto hao shuleni, ukichangia kwa kiasi kikubwa watoto kujiingiza kwenye mambo yasiyofaa ili kupata bidhaa hiyo na mwisho wa siku kukatisha masomo yao.

Alisema kuwa tatizo la wazazi wengi kutokuwa na uelewa wa matumizi ya taulo za kike kwa watoto wao, hivyo kuwahamasisha watumie nyenzo nyingine kama vitambaa, shida nyingine ikiwa ni kutomudu gharama ya kununua bidhaa hizo.

"Watoto wengi wa kike hapa unakuta wamepanga, wanaishi peke yao, hivyo unakuta fedha ya kununua taulo za kike hawana, wanafunzi wengi wanashawishika na zawadi ndogondogo hasa zinazotoka kwa wavuvi, wengine hupata mimba na baada ya hapo hutoweka, hata ukimtafuta kumpata ni ngumu," alisema.

Aliongeza kuwa tatizo ni baadhi ya wazazi kuwa na uchumi na uelewa mdogo wa umuhimu wa taulo za kike kwa watoto wao, hivyo kuwataka watumie nyenzo mbadala.

Mwandishi wa Habari Grace ambaye ni mdau wa masuala ya wanawake, alisema ameamua kutoa msaada huo ili kuhamasisha wanafunzi kusoma na kuepuka vishawishi kwa kisingizio cha kukosa huduma hiyo, akiwafikia wanafunzi wa kike 408 wa shule hiyo.

Kurwa Kadogosa, mmoja wa wanafunzi walionufaika wa msaada huo, alisema wanapitia matatizo mengi wanapokosa bidhaa hizo, hivyo wanaomba wadau wengine kujitokeza kwa wingi kusaidia ili waendelee na masomo yao bila kikwazo.

# ama

ALHAMISI APRILI 4, 2024

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Bingwa tiba aainisha darasa na aonayo, 'undugu' uliozama TB na dawa**



Ukurasa 13

Miaka 14 wanakijiji wanajenga Zahanati wakiishia kwenye boma



Ukurasa 14

**TAASISI NIPE FAGIO, MRADI TAKA SIFURI...**

**Yaja na mfumo unaogeuza taka mtaani bidhaa, nchi jirani yajifunza na kuiga**

KAZI IENDELEE...

# Miaka mitatu inayotumia Sh. Trilioni 1.4 kukabili malaria, kifua kikuu na Ukimwi

**Na Yasmine Protace**

NI hivi karibuni serikali ya Tanzania imepokea Dola za Marekani milioni 602, sawa na Sh. trilioni 1.4, kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa ya malaria, kifua kikuu na Ukimwi katika kipindi cha miaka mitatu inayokoma 2026.

Magonjwa hayo kihistoria, yana kawaida watu wanaougua wakizingatia matibabu yake kwa usahihi, wanaimarika afya zao kwa usahihi na kinyume chake, kutoendana na kanuni za tiba, madhara yako jirani.

Pia, inapoangaliwa kwa undani ugonjwa wa Ukimwi, serikali imekuwa ikipambana nao kwa namna nyingi, ikiwamo kuwapatia elimu wagonjwa wafuate njia hadi mafanikio ya kitabibu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dk. John Jingu, anafafanua hilo jijini Dodoma, katika ufunguzi wa mkutano wa Mkakati wa Utekelezaji Fedha hizo kupitia mradi mpya wa Mfuko wa Dunia Mzunguko wa Saba.

Dk. Jingu anasema, fedha zilizopokewa, zimetokana na jitihada za Serikali Awamu ya Sita, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kuboresha huduma za afya kuwafikia wananchi bila ya kikwazo. Hadi sasa tiba za kifua kikuu, malaria na Ukimwi hutolewa, katika hospitali zote, huku maradhi ya kifua kikuu, yakianzishiwa hadi kliniki zinazowaibua wagonjwa wapya na kuwaingiza katika matibabu.





Kliniki inayotembea kuibua wagonjwa wa kifua kikuu, malaria na Ukimwi, siku ilipozinduliwa na Waziri Ummy Mwalimu, jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

Wizara imekuwa ikieleza jamii ijifunze, hata ikitengua mtazamo wa ugonjwa wa kifua kikuu siyo wa kurogwa na vituo vingi vya afya, wagonjwa wakitibiwa bure, wengi wanaofuatilia matibabu wanapona.

Ni nadharia inayotafsiri pia malaria, ikifafanuliwa mbu jike ndiyo chanzo cha madhara, hasa kwa watoto wachanga, kukiwapo maelezo: "Mkutano huu umeandaliwa kwa wakati muafaka, ili uwe chachu ya kuhakikisha utekelezaji mradi unakuwa na ufanisi uliokusudiwa.

"Lengo ni kuangalia na kufanyia kazi mambo muhimu tuliyojiwekea kwenye mikakati itakayoongoza utekelezaji wa mradi huu."

Dk. Jingu anasema: "Tunatakiwa kuongeza kasi ya utekelezaji na kuongeza uwajibikaji kwa lengo la kuboresha hali ya utoaji wa huduma za afya nchini.

'Ili kufikia malengo hayo, wote tunao wajibu wa kusimamia na kutekeleza ipasavyo mipango tuliyojiwekea na kuwezesha shughuli zote za mradi ambazo zimepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2024-2026."

**WAWAKILISHI**

Mwakilishi wa Marekani, Dk. Etruda Temba, anaishukuru serikali nchini kuandaa mkutano na wadau wa maendeleo, akitoa angalizo la umakini dhidi ya ubadhirifu, fedha zichangie yaliyokusudiwa katika mradi.

Mwakilishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Subisya Kabuje, anasema wao ni wanufaika wa fedha za Mfuko wa Dunia katika Serikali ya Awamu ya Sita, wakipokea shilingi bilioni 39.9 kukamilisha mfumo wa taarifa za afya, kichocheo cha kusimamia huduma ngazi za mikoa hadi vituo vya afya.

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu, akimkaribisha Katibu Mkuu kufungua mkutano, anasema ni lazima nchi ijipange kufikia malengo ya dunia, ili ifikapo mwaka 2026 nchi zijipime kikamilifu mafanikio iliyofikia.

AFYA

# Bingwa tiba aainisha darasa na aonayo, 'undugu' uliozama TB na dawa kulevya

• Askari wanyamapori wapiga kambi vijijini...

**Na Zanura Mollel**

INAPOTAJWA maradhi kifua kikuu au kitaalamu na jina lililozoeleka kwa wengi 'TB' ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria anayeitwa Mycobacterium tuberculosis.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa na dalili zake, ni kama vile kukohoa kwa muda mrefu, homa, kupoteza uzito, pamoja na kutokwa jasho nyakati za usiku.

Kifua kikuu na matumizi ya dawa za kulevya kama vile bangi, cocaine au heroin, zina uhusiano wa karibu, watumiaji wake mara nyingi wako hatarini kupata shida hizi kiafya, kwa sababu ya mfumo wao dhaifu wa kinga na mazingira yasiyo salama kwa watumiaji hao.

Aidha, utumiaji dawa za kulevya unaweza kusababisha uwezekano wa mgonjwa kupuuzia matibabu au kushindwa kufuata ifuatavyo masharti tiba anayopewa mgonjwa wa kifua kikuu, hata kusababisha kuenea maambukizi na ugumu wa kutibu.

### MTAALAM MOUNT MERU

Mtaalam wa afya ya akili katika Hospitali ya Rufani Mountmeru Mkoa wa Arusha, Kitengo cha Methadone kinachohudumia dawa za kulevya, Dk. Muhsin Mnondwa, anaeleza kuwapo uhusiano mkubwa kwa mtumiaji wa dawa za kulevya na kupata maambukizi ya kifua kikuu.

Anasema waraibu wengi wanaopatiwa huduma katika kituo hicho, walibainika kuambukizwa ugonjwa huo, sababu kuu inatajwa ni kuwapo shambulio la magonjwa hatarishi kwao kama vile homa ya ini na virusi vya Ukimwi.

Pia, wataalamu afya wanataja upacha wa TB na Ukimwi, kwamba waraibu wa dawa za kulevya hupata maambukizi ya VVU, hasa kupitia kujidunga sindano, kushiriki ngono zembe na wanapopata maambukizi hayo, kinga ya mwili inashuka kukaribisha kimelea cha TB.

"Mtu mmoja mwenye maambukizi ya ugonjwa wa TB ambaye bado hajaanza matibabu, ana uwezo wa kuambukiza watu 15 kwa siku na kwa wakati mmoja kwa njia ya hewa.

"Hata hivyo makutano katika makundi ya watumiaji wa dawa za kulevya huibuia wagonjwa wapya," anaelimisha Dk. Muhsin, akinena watumiaji bangi wanaathirika mapafu, kutokana na moshi wa dawa hiyo.

Pia, anasema TB ikiambukizwa kwa hewa hiyo chafu, uwezekano wa mtu kupata ugonjwa huo ni mkubwa zaidi.

"Kila binadamu ana vimelea vya TB katika mwili wake. Kinga inaposhuka kutokana na mashambulizi ya magonjwa mbalimbali kama vile saratani, ini na VVU, ugonjwa huo unaanza kushambulia mwili kutokana na uwezo wa kinga kuwa chini," anasema Muhsin.



Aliyekuwa mkuu wa Mkoa Songwe, Tebweta Mgumba, akizindua Kituo cha Waathirika wa Dawa za Kulevya kilichoko Tunduma, mkoani Songwe, Julai mwaka 2021. Picha nyingine, aina tofauti ya dawa za kulevya zenye rekodi kubwa ya kuathiri umma. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



> **Watu 70 hufariki kila siku nchini kutokana na ugonjwa kifua kikuu na wenzao 25,800 hufariki kila mwaka kutokana na ugonjwa huo.**

Anasema kumekuwapo mvutano wa wanasayansi maambukizi ya TB. Lipo, kundi linalosema huambukizwa kwa njia ya hewa na wengine wamefika mbali kusema hata mate yanaambukiza ugonjwa huo.

"Wavutaji wa Bangi wamekua wakishirikiana hata wale wa sigara, bakteria wa TB ni rahisi kupita kwa njia ya mate. Kila siku waraibu wanaongezeka kupata huduma hapa kwa mwezi tunapokea wapya hadi 10," anaeleza Dk. Muhsin.

Vilevile anafafanua kuwa, kituo hicho kwa sasa kinatoa huduma kwa waraibu zaidi ya 700 na tatizo lililopo ni wao kutozingatia matibabu na baadhi kupata madhila, hadi vifo kutokana na matukio ya kihalifu mtaani.

"Waliozingatia matibabu wameshatoka kwenye mfumo, kwa kuwa wamekua sawa. Ikumbukwe hapa tunawahudumia waraibu wengi, wanaofanya makosa ya kihalifu kwa mwaka 2024, tumepokea taarifa vifo vya waraibu wawili," anasema Dk Muhsin.

### RIPOTI YA WHO,2023

Kila tarehe 24 ya mwezi Machi, dunia huadhimisha Siku ya Kifua Kikuu. Takwimu za Shirika la Afya la Duniani (WHO), zilizochapishwa Aprili, 2023, zinaonyesha kuna watu milioni 1.6 (wakiwamo 187,000 wenye maambukizi ya Ukimwi), walikufa kwa ugonjwa wa kifua Kikuu.

Pia, mwaka 2021 watu milioni 10.6 walipata ugonjwa wa TB, kati yao wanaume milioni sita, wanawake milioni 3.4, na watoto milioni 1.2 waliambukizwa maradhi hayo katika maeneo mbalimbali duniani.

Takwimu za WHO zinaonyesha tangu mwaka 2000, kuna watu milioni 74 waliopona kifua kikuu kwa matibabu duniani

### WIZARA YA AFYA

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akifungua Mkutano wa Makatibu Wakuu na Mameneja Mpango wa Programu za Kifua Kikuu kutoka Nchi 15 Barani Afrika uliofanyika kwa siku tatu jijini Arusha, Julai mwaka jana.

Anasema, watu 70 hufariki kila siku nchini kutokana na ugonjwa kifua kikuu na wenzao 25,800 hufariki kila mwaka kutokana na ugonjwa huo.

"Takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa Tanzania ilikuwa na watu 132,000 wanaougua ugonjwa wa kifua Kikuu. Tumeweza kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa huu kwa asilimia 32 na vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kwa asilimia 55," anaeleza Waziri Ummy.

### CHANJO YA TB/UNODC

Ipo chanjo dhidi ya Kifua Kikuu au TB inaitwa 'Bacille BCalmette-Guérin' (BCG) iliyoanza kumtibu binadamu mwaka 1921, ni miongoni mwa chanjo katika programu za utoaji chanjo kwa watoto wachanga.

Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani mwaka 2022, iliyotolewa na Ofisi ya Omoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), inabainisha kuongezeka matumizi ya dawa hizo, ikikadiriwa watu milioni 284 wenye umri kati ya 15 hadi 64, walitumia dawa hizo mwaka 2020.

Idadi ya watumiaji inafanya ongezeko la asilimia 26 kutoka mwaka 2010, ilikuwa na watumiaji milioni 226, huku dawa zilizotumika wakati huo zilikuwa bangi, heroin, methaphetamine, cocaine na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Ripoti imeeleza matumizi ya dawa hizo yaliyosababisha madhara kiafya kwa watumiaji na jamii, ikiwamo ongezeko la maambukizi ya virusi vya Ukimwi, magonjwa ya afya ya akili na homa ya ini.

INAENDELEA UK.13

MAZINGIRA

# Miaka 14 wanakijiji wanajenga Zahanati wakiishia kwenye boma

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

• Hakuna 'senti' serikalini, vilio vyao hadi mikutanoni



Viongozi kijijini Mwamagunguli, wakiwa katika boma ya Zahanati ya kijiji hicho. **PICHA: MARCO MADUHU**

KUKOSEKANA huduma za afya vijijini, imekuwa tatizo kwa wanawake wakikosa elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango, pamoja na kuendelea kujifungua majumbani, na kukwama wakifuata huduma umbali mrefu.

Hicho ndicho kinawakuta wanakijiji wa Mwamagunguli, Kata ya Kolandoto Manispaa ya Shinyanga, hata kulazimika kuanzisha ujenzi wa Zahanati mwaka 2010, lakini ikidimu hatua ya 'renta' miaka 14 haijamaliziwa na serikali.

Sasa wanawake hao wanapaza sauti serikali iwakamilishie Zahanati hiyo, wapate huduma jirani, kama Ester Shija, mkazi wa Mwamagunguli, anayelalamika kutokamilika kwa Zahanati hiyo kijijini kwao, inawaachia wahitaji kinamama shida kubwa ya kufikia huduma za afya.

Anasema huduma za afya wamekuwa wakizipata kijijini humo kutoka hospitali iliyoko Kolandoto, iliyo chini ya kanisa kwamba baadhi ya huduma za uzazi, bado hawazipati ikiwamo ya uzazi wa mpango.

"Sisi kuwa na Zahanati yetu hapa kijijini ni faraja kubwa hasa kwa wanawake, sababu tutapata elimu mbalimbali zinazohusu masuala ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango," anasema Ester.

### WENYE DHAMANA AFYA

Mhudumu Afya Ngazi ya Jamii, Ester Emmanuel, anasema wanawake kijijini hapo hujifungua njiani na wengine majumbani, hali anayoitaja hatari kiafya kwa wahusika.

Anasema anachokifanya kwa wanawake kijijini anawapa elimu sahihi, kwamba wanaposikia dalili za uchungu, wajiandae mapema kuwahi penye huduma za afya hospitalini Kolandoto, ili kumudu umbali uliopo.

Mganga Mfawidhi wa Manispaa ya Shinyanga Dk. Elisha Robert, anataja takwimu za vifo vya uzazi, mwaka juzi ilitokea 16 na mwaka jana 18, huku wakikabiliwa na ugumu wa kukamilisha mabomba ya Zahanati 12 yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

### UONGOZI SERIKALI

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwamagunguli, Makoye Shindayi, anasema mwaka 2010 walihamasisha wananchi kuanzisha ujenzi wa Zahanati kusogeza huduma za afya karibu, hasa wanawake wajawazito na watoto na wakahamasika kutekeleza, hata ujenzi ukafika kwenye 'renta'.

Anasema kiutaratibu, ngazi ya umaliziaji iko kwenye msaada wa kiserikali, lakini daima imetimu miaka 14 haijatekelezwa bado.

"Kwenye zahanati hii wamekuwa wakija viongozi mbalimbali na kutoa ahadi zao kuikamilisha na kisha kuondoka... hatujui nini kinaendelea na kutuachia lawama sisi kwa wananchi," anasema Shindayi.

Anatamka: "Zahanati hii imekuwa kama maonyesho. wamekuwa wakija viongozi mbalimbali, wakiwamo wanasiasa na viongozi wa serikali, na kuahidi kuikamilisha, lakini hakuna kitu!".

Diwani wa Kata ya Kolandoto, Mussa Andrew, anawatia moyo kwamba, Zahanati hiyo kwa mwaka uliopo, ipo kwenye mpango wa ukamilishaji akiwaomba wananchi wawe wavumilivu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, anasema kwamba katika mwaka uliopita wa 2022/2023, Zahanati ilitengewa shilingi milioni 60 kutoka mapato ya ndani, lakini hazikupelekwa na fedha hizo kuelekezwa kwenye miradi mingine, ikiwamo ujenzi wa masoko.

Anasema kwa mwaka wa fedha wa sasa, 2023/2024, serikali kuu imetoa shilingi milioni 50 kukamilisha ujenzi wa zahanati tajwa ya Mwamagunguli, na kwamba wanachosubiri ni mfumo wa kimapato ukamilike.

"Fedha hizi shilingi milioni 50 kutoka serikali kuu haziwezi kuikamilisha zahanati hiyo na kuanza kutoa huduma. Tutakachofanya kama halmashauri, ni kutengea tena fedha kutoka kwenye mapato ya ndani ili ikamilike na kuanza kuhudumia wananchi," anaahidi Mkurugenzi Kagunze.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe akiwa ziara mkoani Shinyanga Februari 23 mwaka huu, akatoa maagizo kwa waganga wakuu, kwamba fedha za miradi ya ujenzi ya afya ikiwamo Zahanati, zisimamiwe kukamilisha miradi husika.

"Haiwezekani Zahanati inajengwa miaka nenda rudi haikamiliki tu. Hii siyo sawa! Waganga Wakuu ambao mtashindwa kusimamia fedha za ujenzi wa miradi ya afya tutawachukulia hatua," anasema Magembe.

Dk. Magembe akawasihi wanawake kujifungua kwenye huduma za kiafya, ili kupunguza vifo vya 'mama na mtoto' vitokanavyo na uzazi.

### RIPOTI UTAFITI 2022

Ripoti ya Utafiti ya Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria ya Mwaka 2022, inasema huduma za uangalizi wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua ni muhimu kwa afya ya mama na mtoto.

Inafafanua asilimia 81 ya watoto waliozaliwa hai kipindi cha miaka miwili kabla ya utafiti, walizaliwa katika vituo vya afya, ikilinganishwa na asilimia 93 ya watoto waliozaliwa wafu.

Vilevile anataja asilimia 85 ya watoto waliozaliwa chini ya uangalizi wa wataalamu wa afya wenye ujuzi.

Ripoti inasema, idadi kubwa ya vifo vya kinamama na watoto hutokea katika saa 48 za kwanza baada ya kujifungua.

Huduma ya uangalizi Mama na Mtoto, baada ya kujifungua ni muhimu, ili kutibu changamoto inayoweza kujitokeza na kuokoa afya yake na mwanawe.

Ripoti inafafanua, kutokana na uboreshaji wa huduma za afya nchini, imesaidia kupunguza vifo vya uzazi kutoka 530 kwa kila vizazi 100,000 mwaka 2015/16 na kupungua hadi kufika vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

## Bingwa tiba aainisha darasa na aonayo, 'undugu' uliozama TB, dawa kulevya

**INATOKA UK.12**

Bangi inatajwa kuwa miongoni mwa dawa za kulevya inayotumiwa zaidi duniani. Hapo kuna watu milioni 209 walibainika kutumia mwaka 2020 sawa na asilimia nne ya watu duniani kote, idadi ya watumiaji ikiongezeka kwa asilimia 23 katika muongo mmoja uliopita.

Matumizi ya dawa za heroin na morphine, watu milioni 61 wakaonekana watumiaji dawa hizo mwaka 2020 sawa na asilimia 1.2 ya watumiaji duniani ,hata hivyo theluthi mbili ya vifo zimehusisha matumizi ya dawa hizo.

Kwenye matumizi ya cocaine, mwaka 2020 watu milioni 21.5 walitumia wakiwa ni wastani wa asilimia 0.4 ya watu wote duniani, kiwango cha uzalishaji kikifika rekodi ya juu mwaka huo, takribani tani 1,982.

### KAMISHNA LYIMO

Kamishna Jenerali Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo anasema kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2023 walifanikiwa kukamata kilo 1,965,340.52 zilizohusisha watuhumiwa 10,522 ikiwa wanaume 9,701 na wanawake 821.

"Kiasi hiki kilichokamatwa cha dawa hizo ni sawa na kiasi kilichokamatwa miaka 11 nyuma kuanzia mwaka 2012" hadi 2022 ambayo ni kilogramu 660,465.4".

Lyimo anasema mamlaka hiyo ilifanikiwa kudhibiti kilo 157,738.55 za kemikali bashirifu zilizoingizwa nchini kinyume na sheria, ambazo zingeweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya.

"Tumefanikiwa kufungua mashauri 765 katika mahakama mbalimbali nchini, mashauri 385 yametolewa hukumu, Jamhuri ilishinda mashauri 355 na kushindwa mashauri 30," anahitimisha.

AFYA

TAASISI NIPE FAGIO, MRADI TAKA SIFURI...

# Yaja na mfumo unaogeuza taka mtaani bidhaa, nchi jirani yajifunza na kuiga

• Hakuna dampo kufurika Dar, Arusha, Zanzibar...

**Na Halfani Chusi**

Ni ufafanuzi wa uthubutu uliofanywa na taasisi ya Nipe Fagio na sasa, serikali ya Zanzibar inautumia kumaliza tatizo la taka kwenye mitaa.

Nipe Fagio, ni taasisi inayojihusisha na 'mfumo wa taka sifuri', kubwa lao ni kutoa elimu katika vikundi vya wakusanya taka, namna ya kuzibadili kuwa bidhaa kama mbolea na chakula cha kuku na samaki.

Wanatekeleza hilo kwa kuzingatia msingi wa kwamba jamii nyingi za kipato cha chini hazina huduma ya usimamizi wa taka na kupambana na matokeo ya uchafuzi wa mazingira ambayo ina athari kubwa kwa afya na maisha yao.

Taasisi hiyo inabainisha kwamba, vikundi jamii vilivyo katika mazingira hatarishi, ni kama vile wanawake, vijana, wakusanya taka, na wakazi wa asili, kwamba lazima wajumuishwe katika suluhu za usimamizi wa taka na wapate fursa, kupitia jukumu hilo.

Utafiti wanaouita kisomi 'Zero Waste to Zero Emissions' ukibeba ujumbe wa kuhamisha taka hadi penye usafi, ukiagazia jiji la Dar es Salaam, ukionyesha mengi kama vile uwezekano wa kupunguza uzalishaji gesi ya methane kwa asilimia 65, kiwango kinachosambazwa nchi nzima.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii wa jiji la Dar es salaam, Saady Khimki anaeleza anavyopokea hilo kwamba:

"Nimefurahishwa sana na kazi nzuri ushirika wa waokota taka wanayoifanya hapa Bonyokwa, ambao wamefadhiliwa na taasisi ya Nipe Fagio.

"Mazingira ni masafi, sijakutana na vifurushi vya taka pembezoni, wala kwenye mitaro wala taka zilizozagaa hovyo. Ningeomba taasisi ya Nipe Fagio tushirikiane kwa pamoja ili kuupeleka mfumo huu katika kata zote za Ilala."

**WENYE MRADI**

Wilyhard Shishikaye, Mratibu wa Mradi wa Sifuri wa Taka Tanzania kutoka taasisi ya Nipe Fagio ana yake: "Katika miaka mitano Nipe Fagio, imeweza kutekeleza mifumo ya Taka Sifuri mikoa mitatu (3) ambayo ni Dar Es Salaam, Arusha na Zanzibar.




Mjumuiko wa wana kikundI cha taka Sifuri, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: HALFAN CHUSI**

> **Lengo ni kuwafungua macho viongozi wa serikali mbinu tunazozitumia kuchakata taka, ili tuweze kupambana na taka ngumu ambazo ni kero kubwa kwa ustawi wa mazingira.**

"Tumesajili chama cha ushirika cha kwanza kuwahi kutokea nchini cha Wakusanya Taka Bonyokwa kilichopo Bonyokwa Dar es Salaam, chenye wanachama zaidi ya 26, hivyo kutengeneza historia kwa vyama rasmi vya wakusanya taka na kuwa daraja kati ya kutambulika rasmi na kazi zao.

"Kuanzia mitaa yenye shughuli nyingi za Dar es Salaam hadi mandhari tulivu ya Arusha na mwambao mahiri wa Zanzibar, Mfumo wa Taka Sifuri umekuwa ukichochea mabadiliko ya mfumo katika usimamizi wa taka," anasema

Anaongeza kuwa, kupitia mfumo huo wamefikia kiwango asilimia 95 ya utenganishaji taka katika maeneo ya Dar es Salaam na Arusha.

Mratibu Shisdhikaye anasisitiza kwamba, iamanisha asilimia 95 ya wanaoishi katika jamii za kipato cha chini, wamekubali mustakabali huo wa kutenganisha taka zao katika makundi yaliyoamuliwa, hata kuwezesha viwango vya juu vya kurejesha taka.

Mwenyekiti wa Wakusanya Taka Bonyokwa, John Nsyenge, ana maoni: "Tumeweza kurejesha asilimia 75 hadi 85 ya taka zote zinazozalishwa katika ngazi ya kaya kupitia mboji, uzalishaji wa chakula cha mifugo na urejelezaji."

Anafafanua kwamba wameweza kudhibiti wastani wa tani 39 za taka kila wmwezi katika kila mtaa wanaouhudumia, zikiwamo tani 30 zilizooza, akijivunia mfumo huo umewezesha kutoa ajira kwa watu 33.

Anasema, kwa sasa wametengeneza mfumo wa ulipaji fedha za ukusanyaji kwa njia ya mtandao kuthibitisha malipo kwa kaya, unaoedana na kufahamishana kwa ujumbe mfupi, kupunguza ulaghai.

"Kuendeleza ushirikiano, tumeweza kuwaleta pamoja watoa huduma, makandarasi, warejelezaji na wakusanyaji taka za kibiashara, kwa kuunganisha na muundo wa kukusanya taka ambao unaendana na mfumo wa taka sifuri na kuongeza ufanisi wa mfumo," anaeleza.

John anataja mafanikio yao, kwamba nchi ya jirani Kenya inayotaka kuiga mfumo wa 'taka sifuri' ulioanza kutumika kwenye mji wao wa Kisumu.

Anasema mfumo huo ni jitihada za kuwezesha mifumo ya kijamii inavyoweza kuigwa kwa mafanikio na kuingizwa katika mazungumzo ya kitaifa, kukuza haki ya kijamii na mabadiliko katika utekelezaji katika miji na nchi nyingi za Afrika.

Pia, anautaja kuwa kielelezo chenye manufaa katika uzalishaji wa ajira, kukabiliana na hali ya hewa, kuongeza ufahamu na haki ya kijamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasis ya Nipe Fagio, Ana Rocha, anasema: "Taka Sifuri sio suluhisho tu; ni dhamira ya mustakabali shirikishi kwa Tanzania, jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko.

"Mfumo wa 'Taka Sifuri' unapendekeza mifumo itakayotatua matatizo ya kimazingira kama uchafuzi wa hali ya hewa, kuruhusu jamii kuelewa mienendo yake na kuchukua hatua stahiki katika kushughulikia matatizo yao.

Anafafanua kwamba mfumo huu unaotekelezwa nchini ni jitihada za wazi unaoshirikisha jamii wenye mafanikio, unavyoweza kuigwa na kuingizwa katika mazungumzo ya kitaifa, kukuza haki ya kijamii, na kuleta mabadiliko katika utekelezaji wa usimamizi wa taka katika miji na nchi nyingi za Afrika.

Anasema mfumo huo unafanya asilimia 15 ya taka kurudi dampo tofauti na awali asilimia yote zilienda dampo hali iliyokuwa inachangia madampo mengi kufurika.

"Wadau tofauti wa mazingira wanapaswa kufahamu kama mfumo huu unatija kuliko unaotumika kwa sasa, mfano mzuri katika maeneo yote ambayo mfumo huo unatumika mafanikio ni makubwa sana ikiwamo Zanzibar.

"Lengo ni kuwafungua macho viongozi wa serikali mbinu tunazozitumia kuchakata taka, ili tuweze kupambana na taka ngumu ambazo ni kero kubwa kwa ustawi wa mazingira.

"Huu ni mfumo ambao unatumika hata nchi za nje katika kudhibiti taka ngumu, kwahiyo ninaamini kama serikali ikilitazama hili kwa undani na kutawanya hakutokuwa na shida tena ya dampo kujaa na hatimaye kumaliza kabisa tatizo la taka" anasema

Matatizo ya mazingira ya kimfumo yanahitaji masuluhisho ya kimfumo ambayo yanajumuisha jamii,yanashughulikia udhalimu wa kihistoria wa kijamii, na yamejengwa kimazingira na kustahimili mabaliko ya hali ya hewa.

Taasisi hiyo inafanya kazi katika mikakati ya nguzo tatu, kukusanya na kupatanisha data, utetezi wa sera, na kuchochea utekelezaji wa vitendo.

Nipe Fagio ni Taasisi iliyojikita katika kuleta mabadiliko ya kimfumo nchini Tanzania na Afrika Mashariki katika sekta ya Mazingira.



# Madaktari watoa sarafu ya 100/- kooni kwa mtoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATAALAM katika Idara ya ENT ya Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa (BMH) Dodoma wamefanikiwa kuitoa sarafu iliyokuwa imekwama kwenye koo la mtoto Agnes Ndunguru (2) kwa muda wa siku sita.

Daktari Bingwa wa Masikio, Pua na Koo wa BMH, Emerenceana Mahulu, alisema BMH imempokea mtoto huyo Alhamisi wiki iliyopita akiwa na changamoto hiyo iliyosabaisha kuteseka kwa maumivu.

Alisema baada ya uchunguzi wa madaktari wamefanikiwa kuitoa sarafu iliyokuwa imekwama kwenye koo la mtoto kwa siku sita kwa kutumia kifaa tiba kinachoitwa _esophagoscopy.

Daktari huyo ambaye pia ni Kaimu Mkuu wa Idara ya ENT ya BMH alisema wazazi wanapaswa kuwa makini na vitu hatarishi kwa watoto kwa sababu vinaweza sababisha kukatisha uhai.

"Napongeza jitihada za madaktari kuokoa uhai wa mtoto wa miaka miwili, siku sita ni nyingi mtoto kukaa na sarafu kooni,"alisema Dk. Mahulu.

Dk. Mahulu alifafanua kuwa sehemu ya koo ilipokuwa imekwama sarafu ilisabisha uvimbe lakini ilikuwa imeacha uwazi kidogo ambayo ilikuwa ikiruhusu vimiminika kama uji, maji juisi kupita.

"Mtoto anaendelea vizuri baada ya matibabu na anaweza kula vizuri kwa sasa. Tumeishamruhusu na tutamuona tena baada ya wiki moja ili kuona maendeleo yake," alisema.

Kwa mujibu wa mama wa mtoto, Juliana Yuda, mkazi wa Kijiji cha Mkoka wilyani Kongwa mkoani Dodoma alisema mtoto wake alitoka kucheza na wenzake Machi 20 mwaka huu, alirudi nyumbani muda wa mchana akiwa analia.

"Mtoto alikuwa hawezi kula kwa muda wa siku sita, alikuwa anashindia uji, juisi na maji tu hali yake ilizidi kuwa mbaya siku," alisema.

Alisema walimpeleka Hospitali ya Wilaya ya Kongwa ambapo alipewa rufaa kuja BMH, baada ya kupigwa picha ya X-ray na kubaini sarafu imekwama kwenye koo.

Alisema baada ya kugundua hilo madaktari walianza harakati za kuokoa maisha ya mtoto huyo na kufanikiwa kuitoa na anaendelea vizuri kiafya.



Mbunge wa Iramba Magharibi ambaye pia ni Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na wananchi wa kata ya Urughu, wilayani Iramba mkoani Singida juzi, akiwa katika ziara yake ya kuhamasisha maendeleo jimboni mwake. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mwenyekiti TCCIA alalamika kuhujumiwa na wajumbe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Dodoma, Khamis Fungameza, amelalamikia kitendo cha baadhi ya viongozi wenzake kutoa rushwa kwa wajumbe wa mkutano mkuu, ili wampigie kura ya kumuondoa kwenye nafasi hiyo.

Fungameza alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuondolewa kwake madarakani kinyume na katiba ya taasisi hiyo.

Hivi karibuni Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Dodoma alizungumza kuhusu uwepo wa vitendo vya ufisadi katika miradi ya taasisi hiyo ukiwemo wa maegesho ya magari Kizota.

Alisema kutokana na ufisadi uliopo hivi sasa kwenye miradi ya taasisi hiyo kunachangia kuiua TCCIA Mkoa wa Dodoma.

Alisema wengi wa viongozi ambao wamechaguliwa kuiongoza taasisi hiyo wapo kwa ajili ya maslahi binafsi, siyo wafanyabishara wenye viwanda au wakulima.

"Upo upigaji mwingi wa fedha za miradi ya TCCIA Mkoa wa Dodoma watu wanakula fedha ambazo zingesaidia kunufaisha wanachama wetu na kutokana na mimi kufuatilia wananitishia na wengine wanasema nije upande wao wa wapigaji.

"Taarifa hizi nimeshampatia Mkuu wa Mkoa ambaye yeye ni mlezi wa taasisi yetu, ameahidi kuzifanyia kazi kwani wapo watu ambao hawataki TCCIA isonge mbele licha ya jitihada zinazofanywa na serikali"alisema.

February 2, mwaka huu TCCIA Mkoa wa Dodoma iliitisha mkutano wenye agenda ya kumjadili mwenyekiti huyo na kuazimia kumuondoa kwenye nafasi yake.

Kwamujibu wa barua iliyoandikwa kwenda TCCIA makao makuu ilieleza kuwa wajumbe wa mkutano mkuu wamedhimia kwa pamoja kumuondoa kwenye nafasi Mwenyekiti wa Mkoa wa Dodoma kutokana na tuhuma mbalimbali.

Barua hiyo ilieleza kuwa moja ya sababu ya kumuondoa katika nafasi yake mwenyekiti huyo ni kushindwa kufanya kazi na kamati ya uongozi.

Sababu nyingine ni kufukuza watumishi bila kufuata sheria, kutaka kufungua kesi polisi kuwashitaki viongozi wenzake na kusababisha kuzua taharuki kwa viongozi wenzake wa taasisi.

Rais wa TCCIA, Vicent Minja, alipotafutwa kutolea ufafnuzi juu ya sakata hilo alidai kuwa mwenyekiti huyo aliondolewa na mkutano mkuu kwa mujibu wa taratibu.

Hata hivyo, alisema kuhusu tuhuma ambazo amekuwa akizitoa za uwepo wa ufisadi ndani ya taasisi zimekuwa hazina Ushahidi, hivyo wao kama viongozi hawawezi kuchukua hatua kwa kitu ambacho hakina vielelezo vya kutosha.

# Mbunge awatangazia neema mamalishe Stendi Kuu ya Mkoa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde ameahidi kuwaboreshea mazingira ya utoaji huduma mamalishe wa Stendi Kuu ya Mkoa wa Dodoma kwa kuwapatia meza na vifaa vya kisasa vya kutolea huduma ya chakula.

Alitoa ahadi hiyo juzi wakati wa mkutano uliowajumuisha wafanyabiashara wadogo, mama lishe na uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma wenye lengo la kutatua changamoto ya uhamishwaji wa wafanyabiashara hao katika maeneo ya Stendi Kuu Dodoma.

"Madhumuni ya ujenzi wa stendi hii ni kutoa huduma ya usafirishaji na pia kuchochea uchumi wa wananchi wa Dodoma kupitia biashara mbalimbali.

"Nishauri uongozi wa Jiji kuwapangia utaratibu mzuri wafanyabiashara hawa wafanye biashara hii kwa muda na baadaye watarejea katika maeneo rasmi baada ya mzunguko wa biashara kuimarika sokoni hapa"alisema

Alisema atawasaidia mamalishe meza nadhifu na vifaa vya kisasa vya kutolea huduma ili wasichafue mazingira ya eneo hilo ili watoe huduma kwa kuzingatia kanuni za afya na usafi wa mazingira.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, John Kayombo alisema amekubali ushauri wa mbunge kwa masharti ya wafanyabiashara hao kupangwa vizuri na kusimamia usafi wa mazingira yao.

Wafanyabiashara wadogo na mamalishe wa Stendi Kuu Dodoma waliishukuru serikali kwa kuwajali na kumpongeza Mavunde kwa kusimamia.

# DC aagiza uadilifu kwa watumishi, usikilizaji kero

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, amewataka watuhumishi wa ngazi za kata wilayani hapa kuonesha uadilifu kwa kusikiliza kero za wananchi katika maeneo yao na kuzitatua.

Alitoa agizo hilo juzi katika kikao kazi cha maofisa tarafa, watendaji wa kata, maofisa ugani, maofisa elimu kata na wakuu wa idara na vitengo.

Gondwe alisema mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya watumishi yanatokana na nidhamu katika kazi, hivyo ni lazima watumishi kuzingatia nidhamu ili kufikia malengo yao ya kazi.

Akizungumzia suala la utatuzi wa kero za wananchi, Gondwe alisema watendaji wote wanapaswa kuanzisha daftari (rejesta) la kusajili kero zilizotokea katika maeneo yao ya kazi na namna walivyozishughulikia ili kuwa na kumbukumbu sahihi.

Aidha, alisisitiza suala la ukusanyaji mapato katika mazao na mifugo na kuwataka maafisa ugani kwa kushirikiana na watendaji wa kata kujituma katika eneo hilo na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

Hivyo, aliwataka maofisa kilimo na mifugo kuisaidia jamii kutofautisha baina ya maeneo ya makazi na maeneo ya malisho Ili kuepuka migogoro inayoweza kutokea.

Gondwe pia aliwataka watumishi kujipanga kwenda juu kimafanikio katika nyanja zote Ili kufikia malengo na maono ya kuifanya Singida kuwa Jiji.

Nao wajumbe wa Kamati ya Usalama Wilaya walihimiza uwajibikaji na uadilifu Ili kufikia matokeo chanya na kurudisha imani kwa wananchi.

Walisema watumishi wanapaswa kutambua nafasi zao kama wasaidizi wa Mkuu wa Wilaya ambao kwa kujituma kwao wataiwezesha Singida kwenda juu kimaendeleo.



# RC ashtuka takwimu udumavu, aagiza utafiti mpya ufanyike

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ameagiza kufanyika upya kwa utafiti wa hali ya udumavu mkoani hapa baada ya kubaini upungufu katika utafiti wa awali.

Mtaka aliyasema hayo wakati wa kikao cha kutathmini utekelezaji wa viashiria vya mkataba wa lishe mkoani hapa kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, mwaka jana.

"Kwa sababu Njombe ina vijiji 381 unafanya utafiti kwa vijiji 48 maana yake hata robo ya vijiji haijafikia na umetoa tathmini ya hali ya lishe mkoa. Hili halijakaa vizuri.

Pale Makete kuna vijiji 98, utafiti umefanyika kwa vijiji vinane na katika vijiji hivyo, umefikia kaya 20 halafu uniambie umefanya utafiti wa lishe Makete?" alihoji.

Mtaka alisema inasikitisha kuona kwamba unakutana na mdau anakwambia kwa yuko mkoani Njombe kumbe yuko kitongoji kimoja tu.

"Tutarudia utafiti kwa yeyote anayetupenda kufanya kazi na sisi ya kuondokana na udumavu ni lazima akubali kuja kwenye aina ya utafiti halisi," alisema Mtaka.

Ofisa Lishe Mkoa wa Njombe, Bertha Nyingu, alisema pamoja na jitihada za kupambana na udumavu, taarifa sahihi zinakuwa shida kutokana baadhi ya wauguzi katika vituo vya afya kutopima urefu kwa sababu ya kukosekana kwa vibao.

"Kama tungekuwa tunapima vizuri na vibao tunavyo hata matokeo tungepata ambayo yanaakisi uhalisia," alisema Nyingu.

Naye Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Gladness Machange, alisema kati ya vijiji 45, utafiti ulifanyika katika vitongoji saba, vijiji saba na kata sab ana kuzifikia kaya 280 na watoto 279.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, alizitaka asasi kujikita katika kuonana na wananchi sambamba na kuwapa elimu na madhara ya udumavu.



Wafanyabiashara maarufu machinga wakifanya shughuli zao kwenye njia ya waenda kwa miguu, eneo la Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa wapita njia. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bil. 19/- kutekeleza miradi maendeleo Ludewa

**Elizabeth John,** LUDEWA

ZAIDI ya Sh. bilioni 19 zimetolewa na serikali ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani Ludewa mkoani Njombe katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Fedha hizo zinatarajiwa kutatua changamoto kwenye sekta za elimu, afya, maji na kilimo.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, aliyasema hayo jama wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi kwa waandishi wa habari wilayani hapa.

Mwanziva alisema kwa wilaya ya Ludewa maendeleo ya kiuchumi yanazidi kupiga hatua kwa kasi ikiwa ni tofauti na miaka iliyopita.

"Katika miaka hii mitatu, Rais Samia maono na malengo yake ni kuzidi kuona Tanzania inasonga mbele na hapumziki kushoto na kulia kila siku anaangaika kwa ajili ya taifa letu," alisema.

Hata hivyo alisema viongozi wa chama na serikali wilayani hapa wameungana ili kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi. "Ujenzi wa barabara unaendelea lakini maboresho mbalimbali yanaendelea ili shughuli za kiuchumi ziweze kufanyika kwa tija," alisema Mwanziva.

Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ludewa, Gervas Ndaki, alisema Dk. Samia amewafundisha kwa vitendo siasa za maridhiano na ushirikiano.

"Na hii inatokana na ilani ya uchaguzi ya CCM ibara ya 108 hadi ibara ya 130 ambayo inazungumzia sehemu kubwa ya utawala bora, utawala wa sheria na utawala wa kujali wananchi hii ni sura ya sita katika kitabu chetu cha ilani ya chama chetu cha mapinduzi," alisema Ndaki.

Ndaki alisema Rais. Samia ametekeleza ilani ya CCM kwa kiwango cha hali ya juu kulinganisha na marais wa awamu zilizopita. "Amefanya kazi kubwa sana, kwanza amekuwa anatafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha miradi inatekelezwa na sisi wote ni mashahidi huko nyuma tulikuwa tunachanga kwa ajili ya kujenga madarasa lakini sasa hivi shule za kisasa zinajengwa kwa fedha ya serikali," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratius, alisema halmashauri imepokea Sh. bilioni 19.9 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Fedha hizi zimejikita katika sekta ya afya, elimu msingi na sekondari lakini pia na sehemu ya utawala. Kwa hiyo fedha zote hizi tumezipokea kwa maana ya utekelezaji. Upande wa afya, Sh. bilioni 4.6 zitajenga miundombinu mbalimbali ikiwamo zahanati na dawa," alisema,

Deogratias alisema halmashauri hiyo imepokea pikipiki kwa ajili ya maafisa ugani ambazo zitawawezesha kuhudumia wakulima mmoja mmoja na wafugaji.

# Polisi yaonya matumizi ya moto ndani ya nyumba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe limewaonya wananchi mkoani hapa na kuwataka kuacha utamaduni wa kuota moto kwa kutumia majiko ya mkaa ndani ili kuepuka vifo kutokana na tabia hiyo.

Wito huo ulitolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi (ACP) Mahamod Banga, wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu.

Kamanda Banga alisema kuweka jiko la mkaa ndani ni hatari kwa afya ya mwanadamu kwa sababu linaweza kumsababishia kifo.

"Kumbuka mkaa ni hatari kwa afya ya mwanadamu kwa sababu ya ile sumu ya mkaa ni mbaya sana ukivuta muda mrefu inakusababishia kifo," alisema.

Kamanda Banga alisema kutokana na hali ya baridi ya mkoa wa Njombe, tayari wananchi wamejiwekea utamaduni wa kuota moto kwa kutumia majiko ya mkaa ndani hali ambayo ni hatari.

Baadhi ya wananchi mjini Njombe walisema sababu kubwa ya wakazi mkoani humo kutumia majiko ya mkaa ndani kwa ajili ya kuota ni kutokana na hali ya hewa ya baridi.

Mmoja wa wananchi hao, Gaspar Tweve, alisema hali ya hewa ya Njombe ni ya baridi na ujenzi wa nyumba wa zamani ulikuwa unazingatia kuwapo na sehemu maalumu ya kukoka moto lakini hivi sasa walio wengi wanajenga kisasa kwa kuiga mitindo ambayo inafaa zaidi katika maeneo yenye joto.

"Labda elimu itolewe kwamba ujenzi wa nyumba katika maeneo yenye baridi uzingatie jeografia ya maeneo husika na hali ya hewa," alisema Tweve.

Naye Seif Msingwa alisema hali ya hewa ya Njombe ya baridi ndiyo inayochangia watu kuota moto kwenye vigae (jiko) ndani licha ya tahadhari mbalimbali zinazotolewa



# Pensheni za wazee sasa kupitia benki

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya Salum, amesema wazee wote wanaolipwa fedha za pensheni jamii watafunguliwa akaunti ili malipo yapitie benki na kuepusha matukio ya udanganyifu na vitendo vya utapeli.

Waziri Mkuya alisema hayo jana, alipofanya mazungumzo na wazee wanaopokea fedha za pensheni jamii katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni, Mjini Unguja na kuwakutanisha viongozi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Alisema kwa muda mrefu serikali imekuwa ikifanya malipo ya pensheni jamii kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70 katika utaratibu ambao si rasmi wa kulipa mikononi kupitia katika vituo walivyokubaliana na wazee.

Dk. Mkuya alisema utaratibu huo kwa kiasi kikubwa umekuwa na changamoto nyingi ambazo kwa nyakati tofauti zimeibua malalamiko ikiwamo baadhi ya wazee kushindwa kufikiwa na kupata fedha hizo.

Alisema kwa sasa serikali imeamua wazee wote wanaostahili kulipwa pensheni jamii, kufungua akaunti kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa ajili ya kupata malipo halali.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeanza mfumo wa malipo ya fedha za pensheni jamii kwa wazee kwa njia ya benki hatua ambayo ni salama yenye uhakika wa fedha za wazee kuwafikia moja kwa moja," alisema.

Aidha, alisema mfumo wa malipo ya pensheni jamii kwa wazee wastaafu kupitia benki utaondosha udanganyifu ambao uliwahi kufanywa na watendaji wa wizara ambao si waaminifu.

Naye Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Rikizi Pembe Juma, alisema uamuzi wa kuwafunguliya akaunti wazee wanaolipwa fedha kupitia pensheni jamii ni sahihi na wenye lengo la kuondoa usumbufu kati ya watendaji wa wizara pamoja na wazee kwa ujumla.

Alisema uamuzi wa kuwalipa wazee pensheni jamii unatokana na serikali kutambua mchango mkubwa wa wazee ambao walifanya kazi kubwa ikiwamo katika kuleta uhuru pamoja na kutunza familia ambazo matokeo yake ndiyo jamii iliopo sasa.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, alizipongeza wizara hizo kwa kazi kubwa zinayofanya katika kutekeleza na kusimamia jukumu la kulipa pensheni jamii ya wazee waliofikisha umri wa miaka 70.

Alisema wazee wanatakiwa kuenziwa, hivyo kitendo cha wizara mbili kuweka mazingira mazuri ya kulipwa pensheni jamii kinastahili kuungwa mkono.

Zaidi ya wazee 25,000 wanalipwa pensheni jamii na serikali ya Zanzibar na miongoni mwa vigezo muhimu ni kufikia umri wa miaka 70 ambayo kwa sasa imeongeza na kufikia kiwango cha Sh. 50,000 kwa mwezi.

# SMZ yaapa kuwaenzi waasisi Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuwaenzi viongozi waasisi wa Mapinduzi ambao wametumia muda mwingi wa maisha yao kuikomboa Zanzibar kutoka kwa watawala wa kikoloni.

Hayo yalisemwa kwa nyakati tofauti na viongozi wa serikali akiwamo Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, alipofika katika kaburi la aliyekuwa mwasisi wa Mapinduzi, Said Iddi Bavuai, Shakani wilaya ya Magharibi Unguja kwa ajili ya kumwombea dua.

Alisema Bavuai atakumbukwa kutokana na ushujaa wake mkubwa kwa kushirikiana na viongozi wengine akiwamo Jemedari wa Mapinduzi ya Januari 12, 1964, Sheikh Abeid Amani Karume, kuuangusha utawala wa Kisultani wa Oman.

Soraga alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kuwakumbuka viongozi hao kutokana na mchango mkubwa ambao umewawezesha wananchi wa Zanzibar kuwa huru katika nchi yao na kufanya shughuli za uzalishaji mali na maendeleo.

"Wazanzibari tuko katika wiki ya kuwakumbuka viongozi mashujaa ambao walifanya kazi kubwa katika kuleta uhuru wa Zanzibar kutoka kwa wakoloni," alisema Soraga.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uwezeshaji na Uchumi, Sharif Ali Sharif, alifika Mkwajuni mkoa wa Kaskazini Unguja na kuzuru kaburi la aliyekuwa Waziri kiongozi wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ramadhan Haji Faki, aliyefariki dunia miaka mitano iliopita.

Sharif alisema Faki atakumbukwa kutokana na ushujaa wake alipotumia mbinu mbalimbali kufanikisha Mapinduzi ya Januari 12, 1964 baada ya wanamapinduzi wazalendo kuivamia kambi ya ulinzi ya wakoloni, Bomani mjini Unguja.

Akitoa wasifu wake, Sharif alisema Faki alikuwa kiongozi shupavu na jasiri ambaye uzoefu wake ulisaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha Mapinduzi ya Januari 12, 1964.

Pia alisema Faki alikuwa miongoni mwa viongozi wa mwanzo waliounda jeshi la kwanza la ukombozi la Zanzibar baada ya Mapinduzi kabla ya kuungana na kuitwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kutokana na Tanganyika na Zanzibar kuungana na kuzaliwa taifa jipya la Tanzania Aprili 26, 1964.

Aidha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Ali Suleiman Ameir, alifika katika kijiji cha Mwache Alale kwa ajili ya kumwombea dua mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, Meja Jenerali Said Abdalla Natepe aliyefariki dunia mwaka 2010.

Ameir alimtaja Jenerali Natepe kuwa miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Mapinduzi 14 walioshiriki katika Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964. Pia alishika nafasi mbalimbali katika serikali ya Muungano ikiwamo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Familia za wananchi ambao waliotembelewa wazee wao waasisi walisema wamefurahishwa na utaratibu uliowekwa na serikali kwa kuwakumbuka viongozi hao na kutambua mchango mkubwa kwa Zanzibar.

Hii ni wiki ya kuwaombea dua viongozi na waasisi wa Zanzibar ambao walifanya kazi kubwa katika kuleta ukombozi wa Zanzibar ambayo itafikia kilele chake Aprili 7, mwaka huu, ambayo ni siku ya kitaifa ya mashujaa.

Siku hiyo ni kumbukizi ya Jemadari Mkuu wa Mapinduzi ya Zanzibar na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, ambaye aliuawa tarehe kama hiyo mwaka 1972 wakati huo akiwa Rais wa Zanzibar na Mwkamu wa kwanza wa Rais wa Tanzania.



Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo Taifa ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kushoto), akishiriki futari na Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, aliyoindaa, jijini Dar es Salaam juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wanufaika kilimo vitendo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Dk. Mohamed Dhamir Kombo, amesema taasisi hiyo ina jukumu la kufanya utafiti na kutoa taaluma ya sayansi ya kilimo kwa vitendo.

Amesema lengo ni kupata misingi bora ya elimu ya kilimo sambamba na kuwajenga kuwa wataalamu wazuri wa fani mbalimbali baadaye.

Dk. Kombo aliyasema hayo jana katika ofisi za taasisi hiyo, Kizimbani, alipokuwa akiwaaga na kuwakabidhi vyeti wanafunzi waliopata mafunzo ya vitendo kwa miezi mitatu kutoka Chuo cha Kilimo cha Kaole, Bagamoyo.

Alisema taasisi hiyo imekuwa na utaratibu mzuri wa kutoa nafasi za kujifunza kwa vitendo sayansi ya kilimo kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali kuanzia shule za maandalizi, msingi, sekondari wa ndani na nje ya Zanzibar ili kujenga wataalamu bora ambao watasaidia kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo.

Pia alisema pamoja na kupata taaluma kwa wanafunzi hao pia wanapata nafasi za kufanya ziara za kujifunza ambazo zinawajengea uwezo na hamu ya kuipenda fani ya kilimo ambayo inawashajihisha kuiona ni kazi yenye tija kwao na taifa kwa ujumla.

Naye Ofisa Mafunzo wa ZARI, Maryam Hamdu Simai, alisema mkakati maalum wa taasisi hiyo hutoa fursa ya kujifunza kwa vitendo kupitia maabara ya afya ya udongo, aina za mazao, udhibiti wa wadudu pamoja na uzalishaji wa mazao.

Mwanafunzi George Ndomboka, kwa niaba ya wanafunzi wenzake, alimshukuru Mkurugenzi Mkuu wa ZARI, kwa kupata fursa ya kujifunza kwa vitendo masuala ya utafiti wa kilimo kwa sababu mategemeo yao ni kuwa wataalamu wazuri.

Kwa niaba ya wenzake, aliahidi kuyafanyia kazi yale yote waliyojifunza pamoja na kuwa mabalozi wazuri kwa wanafunzi wengine.

Jumla ya wanafunzi 2,984 kutoka shule na vyuo 127 wametembelea na kupata fursa ya mafunzo katika taasisi hiyo katika mwaka 2023/2024.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SHANGWE ZAKARIA KALINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **MC 738 CKM** AINA YA BOXER YENYE JINA LA USAJILI **MOHAMED ENTERPRISES**, YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/4011/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

Ndugu **MOHAMED JUMBE MOHAMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya trailer yenye Namba za usajili: **T 739 CFC** na Chassis Namba: **C023420.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa katika kituo cha Polisi kilicho karibu nawe. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/2036/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVA KACZOROWSKI NYANYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya RAV4 yenye usajili namba **T 271 BSB.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/52470/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDALLAH ALLY NYIKA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari(Mitsubishi canter) yenye namba za usajili **T 909 ATG** (CHASSIS NO. **FE637E530930,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **PHQ/MOR/MOR/7615/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA KISARAWE**

**SHAURI LA ARDHI NAMBARI 16 LA 2024**

**MWAJUMA SHOMARI SAMAYA.........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **JOSEPH J. NINGA**
2. **IDDY SHOMARY MAGONGO**
3. **JUMA SAIDI NASORO**
4. **GEOFREY ELIA MWALIAJE............................................WAJIBU MAOMBI**

**TANGAZO**

Wewe **JOSEPH K. NINGA, IDDY SHOMARY MAGONGO, JUMA SAIDI NASORO & GEOFREY ELIA MWALIAJE** popote pale mlipo mnaamriwa na baraza hili la ardhi na Nyumba Kisarawe kuhudhuria hapa kwenye Baraza mnamo tarehe 17.04.2024 kama hamtahudhuria basi Baraza hili litasikiliza upande mmoja na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 mwezi April, 2024

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
KISARAWE - PWANI

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MANYONI**

**MAOMBI NA. 52 YA 2023**

**BAINA YA**

**DAVID MPANDAGOYA ........................................ MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **MASUMBUKO ROMANI................ MJIBU MAOMBI NA. 1**
2. **PASKALI LUMASHI............................MJIBU MAOMBI NA. 2**
3. **JOWELY SAHANI.............................MJIBU MAOMBI NA. 3**

**KWA: PASKALI LUMASHI**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria tarehe 10/06/2024 saa 2:30 asubuhi . kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni ya kutajwa kwa shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIA:**
Kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itaendelea kusikilizwa upande mmoja.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya Baraza hili leo tarehe 06/03/2024.

O.Y. MBEGA
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MANYONI

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26732 OF 2023**

**In the Matter of Estate of the Late EDWARD RAFAEL NGABONA**

**and**

**In the Matter of Application for letters of administration by HERRIET EDWARD NGABONA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 day of 02 2024

Dated at DAR ES SALAAM this 4 day of 12 2023

Senior Resident Magistrate

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya GEITA**
**Kituo cha BUGANDO**

**Shauri la madai Na 21/2024**

**Jina la Mdai SHABANI JOSEPH**

**Jina la mdaiwa SIJAONA MALIMA 2. MANENO MASALU**

**KUITWA SHAURINI**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:- MANENO MASALU**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) **YA TSH 634,500/= LAKI SITA ELFU THELATHINI NA NNE MIA TANO.**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 10 Mwezi 4 Mwaka 2024 saa 2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujiteta.
**ANGALIZO:** Kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 2 mwezi wa 4 mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
BUGANDO

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 58 MWAKA 2024**

**SULEIMAN M. LUTEGO...............................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**AZIZA ABDALLAH GANZEL.............MJIBU MAOMBI**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

**KWA: AZIZA ABDALLAH GANZEL**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 07 mwezi 05 mwaka 2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mhe. O. MBEGU Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako/mwakilishi wako pasipo kukosa na ulete utetezi wako ndani ya siku ishirini na moja (21) toka tarehe ya kupokea kuitwa shaurini.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/ Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 28 Mwezi 03 Mwaka 2024.

MWENYEKITI

---

**FOMU MADAI – 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ...........TANGA.........**

**Kituo cha .........MJINI TANGA ...... ....Mkoa..........TANGA.........**

**Shauri la Madai la Ndoa Na... ......TALAKA.........../2024.........**

**Jina la Mdai.....SWAHIBA MIRAJI......Jinsia............KE.........**
**Makazi ..........KISOSORA...Umri ................26...............**

**Anuani ya Makazi ............13...... ....Kazi........... .... MJASIRIAMALI.......**

**Jina la mdaiwa YUSUPHU MOHAMEDI ...........Jinsia.......ME .......**

**Makazi ............MAKORORA ................. Umri ....39.....................**

**Anuani ya makazi ...................kazi.........MJASIRIAMALI......**

**Simu ............... 0786955640 ................Barua pepe ...................**

**HATI YA MADAI**
**(Kanuni ya 15(1)(2) ya Kanuni za Mashauri ya Madai Mahakama za Mwanzo)**
**.................HABARI YA MADAI YA TALAKA.................**

..............................................................................................
Nathibitisha kwamba yote niliyoeleza hapo juu ni kweli kwa kadri nijuavyo.
Tarehe...02...Mwezi ...04 ...Mwaka...2024... Mahali ... Mahakama

---

## TAARIFA KWA UMMA

Tunategemea mzigo mkubwa **(Wide load)** kutoka mpaka wa Holili kupitia **Shrimatunda** hadi **Bonite Bottlers Limited** kati ya tarehe 05/4/2024 na 18/4/2024

- Namba ya Gari: **KBS037J /ZB2799,** Ukubwa wa Gari( Size) : Length 18M X Height 5M X Width 3.0
- Namba ya Gari: **KBZ903A /ZD4287,** Ukubwa wa Gari( Size) : Length 22M X Height 5.3M X Width 3.5

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Marekani, Uingereza zakosa uvumilivu

**WASHINGTON,** Marekani

MATAIFA makubwa yanayoiunga mkono Israel katika vita yake na Hamas, yameonekana kuigeuka nchi hiyo na kuilaani kutokana na mauaji ya wafanyakazi saba wa misaada.

Rais wa Marekani, Joe Biden, ametoa kauli kali dhidi ya Israel kwa kueleza kuwa amekasirishwa na kuvunja moyo kutokana na matendo yake.

Rais Biden, aliishutumu nchi hiyo kwa kutochukua hatua za kutosha kwa ajili ya kuwalinda wafanyakazi wa misaada na raia wa Palestina.

Baada ya tukio hilo, Israel iliahidi kufanya uchunguzi huru kufuatia maneno makali na shutuma kutoka nchi za Uingereza, Marekani, Canada, Australia na Poland ambazo zote zimepoteza raia wake katika shambulizi hilo lililofanyika Jumatatu kaskazini mwa mji wa Gaza.

**Watu hao waliouawa katika shambulizi hilo la anga walikuwa wakifanyakazi na World Centre Kitchen (WCK) katika Jiko Kuu la Dunia (WCK).**

Hata hivyo, Rais wa Israel, Isaac Herzog, aliomba radhi kutokana na vifo hivyo.

Watu hao waliouawa katika shambulizi hilo la anga walikuwa wakifanyakazi na World Centre Kitchen (WCK) katika Jiko Kuu la Dunia (WCK).

Rais Biden, alitaka Israel iwajibike kufanya uchunguzi wa haraka na matokeo yake yawekwe hadharani.

Alisema hali ya sasa usambazaji wa misaada Ukanda wa Gaza umekuwa mgumu sana kwa sababu Israel haijafanya vya kutosha kuwalinda wafanyakazi wa mashirika ya kimataifa wanaojaribu kutoa msaada unaohitajika kwa raia.

Katika lugha yake kali kuitoa tangu vita hivyo kuanza kiongozi huyo, alisema Marekani mara kwa mara iliitaka nchi hiyo kusitisha vita lakini inakaidi.

"Marekani mara kwa mara imekuwa ikiitaka Israel kusitisha operesheni zao za kijeshi dhidi ya Hamas, ili kuepusha maafa ya raia," alisema Rais Biden.

Kwa upande mwingine nchi ya Uingereza imechukua hatua zisizo za kawaida kwa viongozi wa Israel.

Hatua ya kwanza ni kumuita balozi wa Israel kwa ajili ya mazungumzo na Ofisi ya Mambo ya Nje, ikiwa ni mara ya kwanza baada ya miaka 12.

Pia Waziri Mkuu, Rishi Sunak alifanya mazungumzo ya wazi na Benjamin Netanyau usiku wa kuamkia jana.

Katika mazungumzo hayo, Sunak alimwambia Netanyahu kuwa amechukizwa na mauaji hayo, na kwamba wafanyakazi wengi wa mashirika ya kutoa misaada na raia wamefariki jambo ambalo linazidi kutovumilika.

Mazungumzo ya aina hiyo si rahisi kutokea kati ya viongozi wa nchi hizo mbili washirika.

Serikali ya Uingereza pia iliweka wazi kuwa inataka ulinzi zaidi kwa raia, kuweka masharti kidogo ya usambazaji misaada ya kibinadamu na kuchukuliwa kukarabati miundombinu muhimu kama hospitali. **BBC**

## Sheria Bima Afya kwa Wote kuanza kutumika mwezi huu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeanza maandalizi ya kutumika kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kuainisha baadhi ya vifungu ambavyo vinaweka mifumo imara ya kutekeleza bima ya afya kwa wote vitakavyoanza kutumika kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Furaha Matondo aliyetaka kujua lini Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote itaanza kutumika.

Dk. Mollel alisema Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ilipitishwa na Bunge Novemba Mosi, 2023 na Rais aliidhinisha sheria hiyo Novemba 19, 2023 na ilichapishwa katika gazeti la Serikali la Desemba Mosi, 2023. Alisema serikali imeanza maandalizi hayo na kwa mujibu wa kifungu cha kwanza cha sheria hiyo, waziri anaweza kuteua baadhi ya vifungu vya kuanza kutumika.

"Baadhu ya vifungu ambavyo vinaweka mifumo imara ya kutekeleza bima ya afya kwa wote vimeshaainishwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sheria itatangazwa kuanza kutumika kabla ya mwisho wa mwezi wa nne (Aprili) mwaka 2024 kwa tarehe itakayotajwa," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kusaidia wajane ambao hawana uwezo wa bima ya afya katika utekelezaji bima hiyo.

"Maeneo ya miji mikubwa kama Mkoa wa Mwanza kuna wimbi kubwa la watoto yatima na watoto wa mitaani. Ni upi mkakati wa serikali wa kusaidia watoto hao wapate bima ya afya ili kuwa na afya bora?" alihoji.

Dk. Mollel, akijibu maswali hayo, alisema utaratibu wa kusaidia wasio na uwezo kuwa na bima ya afya uliopitishwa na bunge utatumika kwa kundi la wajane.

Hata hivyo, alisema kwa kundi la watoto wa mitaani, jamii inapaswa kushirikiana na serikali kuwaondoa na kuwarudisha kwenye familia zao ili kuwa na utaratibu mzuri.



Baadhi ya majengo yakiwa yamelala upande baada ya tetemeko la ardhi kuikumba Taiwan jana asubuhi. **PICHA: IMAGO**

## Tetemeko la ardhi laikumba Taiwan

**TAIPEI,** Taiwan

WATU saba wamethibitika kufariki na wengine zaidi ya 800 wamejeruhiwa baada ya tetemeko kubwa la ardhi kuikumba Taiwan.

Tetemeko hilo lenye ukubwa wa 7.4 kipimo cha Richter, limesababisha uharibifu mkubwa wa majengo na miundombinu mbalimbali ikiwamo barabara.

Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Taiwan(CWA), ilisema kuwa tetemeko hilo la ardhi lililotokea Jumatano asubuhi na Shirika la Utafiti wa Jiolojia la Marekani, USGS lilieleza chimbuko la tetemeko hilo kilomita 18 kusini mashariki mwa kaunti ya Hualien, katika kina cha kilomita 34.8.

Idara ya Kitaifa ya Zimamoto zilieleza kuwa takribani majengo 26 yameanguka, huku zaidi ya nusu ya idadi hiyo yakiporomoka kwenye kaunti ya mashariki ya Hualien.

Kulingana na idara hiyo, vifo vyote vimetokea katika kaunti hiyo, na kwamba hadi jana watu 820 wamejeruhiwa. Aidha, ripoti zinaeleza kuwa waokoaji wanatumia ngazi kuwaokoa watu na kuwapeleka maeneo salama.

Picha na video zilizorushwa kwenye televisheni za Taiwan zimeonyesha jinsi maghorofa mengi kwenye kaunti ya Hualien na kwengineko yakiporomoka, kutitia na mengine yakiwa yamepinda.

Mmoja wa wakazi wa Taipei, Fu Zhong Mei, amesema kulikuwa na hali ya taharuki wakati tetemneko hilo linatokea.

"Nilipogundua kuwa ni tetemeko, haraka nilivaa nguo na viatu, kisha nikamchukua mwanangu tukakimbia na kushuka ngazi. Sijachukua kitu chochote," alisema Fu.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Matetemeko cha Taipei, Wu Chien-fu alisema tetemeko hilo limesikika Taiwan kote na visiwa vya jirani.

Wu alisema watu wanapaswa kuchukua tahadhari na kuwa tayari kuondolewa kwenye makazi yao kutokana na athari ya tetemeko hilo.

Watu wengine 60 wamekwama kwenye njia za chini ya ardhi ya Jinwen, barabara kuu ambayo inaiunganisha miji ya Suao na Hualien. **DW**

## Bei moja mafuta petroli, dizeli nchi nzima yanukia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inafanya tathmini ya uwezekano wa kupanga bei moja ya bidhaa za petroli nchi nzima.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo.

Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kuweka utaratibu ili bei ya mafuta ya dizeli na petroli iwe moja nchi nzima. Akijibu swali hilo, Judith alisema utaratibu huo ulikuwa unatumika miaka ya nyuma na ulikwama kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo sera na usimamizi.

"Hivyo, wafanyabiashara wa mafuta waliruhusiwa kupanga bei za bidhaa za mafuta kuendana na ushindani wa soko. Tathmini hiyo itakapokamilika, serikali itaweza kujiridhisha iwapo utaratibu huu una tija ikiwa ni pamoja na kujua namna bora ya kuusimamia ili kuhakikisha changamoto zilizojitokeza kipindi cha nyuma hazijirudii," alisema.

Mbunge huyo alihoji pia serikali inatarajia kukamilisha lini tathmini hiyo ili wananchi walio nje ya Dar es Salaam wanufaike na imejipangaje kutatua vikwazo vya nyuma vilivyojitokeza.

Naibu Waziri Judith, akijibu swali hilo, alisema tathmini hiyo ilitokana na maelekezo ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko kwamba ifanyike haraka na itakamilika hivi karibuni.

Alisema tathmini hiyo itaeleza vikwazo vilivyojitokeza awali na namna ya kujipanga kuwa na utaratibu mzuri utakaotekelezeka.

# ZAHERA KICHEKO NAMUNGO FC IKITINGA ROBO FAINALI FA

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Mwinyi Zahera, amesema amefurahi kuona timu yake imekuwa ya kwanza kufuzu hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA na kuongeza hiyo imetokana na wachezaji wake tayari wameshaanza kumwelewa na kufanya yale anayowaagiza.

Namungo ilisonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuifunga Kagera Sugar penalti 5-3 katika mechi ya hatua ya 16 Bora iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, Lindi juzi usiku.

Timu hizo zililazimika kufika hatua ya penalti baada ya kutoka sare ya bila kufungana.

**"Nimefurahi tumeingia robo fainali, tumekuwa timu ya kwanza kutinga hatua hii, nadhani ni mwanzo mzuri, kwa sasa wachezaji wangu wameshaanza kunielewa nini nahitaji, imewaweka vizuri wachezaji wangu nao kuanza kujiamini kuelekea katika mechi za Ligi Kuu," alisema Zahera.**


Namungo iliweka wavuni penalti zote kupitia kwa Derreck Mukombozi, Ibrahim Mkoko, Ayoub Semtawa, Hassan Kibailo na Frank Domayo huku zile Kagera Sugar zilifungwa na Mubarack Amza, Obrey Chirwa na Abdallah Seseme wakati ile ya Geofrey Manyasi, iligonga nguzo ya pembeni na kurudi uwanjani.

Kwa sasa Namungo itaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC itakayochezwa Aprili 13, mwaka huu.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Namungo inashika nafasi ya tisa ikiwa na pointi 23 baada ya kucheza michezo 21 mpaka sasa.

Wakati huo huo nyota wa Namungo, Hassan Kabunda, ameteuliwa kuwa Mchezaji Bora wa mechi hiyo ya michuano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake hupata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.






Kiungo mshambuliaji wa Namungo FC, Hassan Kabunda (kushoto), akiwa ameshika hundi ya mfano ya Sh. 500,000 baada ya kutangazwa Mchezaji Bora wa mechi ya hatua ya 16 Bora ya Kombe la FA dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, Lindi juzi usiku. Namungo ilishinda penalti 5-3. **PICHA: MTANDAO**

# Mtibwa Sugar FC yaota Nane Bora

Na Saada Akida

LICHA ya timu yake kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema anataka kuona kikosi chake kinatinga hatua ya Nane Bora ya mashindano ya Kombe la FA (Kombe la CRBD Bank Federation).

Mtibwa Sugar wanajiandaa kuikabili Azam katika mchezo wa hatua ya 16 bora wa michuano ya Kombe la FA utakaochezwa Jumapili katika dimba la Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Katwila alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo licha ya kuwa katika kipindi kigumu anaamini watafanya 'maajabu' katika mechi hiyo.

Katwila alisema amefanyia kazi makosa yaliyojitokeza na sasa wako tayari kwa mchezo huo.

Alisema wanatambua ubora wa Azam na kwa sababu hiyo wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kusonga mbele.

"Hakuna mechi rahisi katika hatua hii ambayo kila timu iliyopo iko vizuri, anaimani na vijana wake watafanya vyema kwa kuyahamisha yale ya mazoezi katika uwanja wa mechi," alisema kocha huyo.

Aliongeza wanatakuwa kuongeza umakini kwa sababu watacheza ugenini lakini akiwakumbusha wachezaji wake kutumia kila nafasi itakayopatikana.

## Kriketi kufanya mchujo wa U-18

Na Shufaa Lyimo

CHAMA cha Kriketi Tanzania (TCA), kimesema kinatarajia kufanya mchujo ili kupata wachezaji 30 watakaounda kikosi cha Timu ya Taifa ya vijana ya Wanawake wenye umri chini ya miaka 18, imeelezwa.

Kwa sasa wachezaji 60 wako kambini wanaendelea na mazoezi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa TCA, Hamisi Abdallah, alisema wachezaji hao 30 watakaoteuliwa watawakilisha nchi katika mashindano ya kuwania kufuzu michuano ya Kombe la Dunia itakayochezwa Agosti, mwaka huu nchini Uganda.

Abdallah alisema wachezaji hao walioko kambini kwa sasa wanaendelea na mashindano ya ndani yatakayomalizika keshokutwa hapa jijini.

Aliongeza anafurahi kuona mwamko wa wachezaji kushiriki kriketi umebadilika tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita washiriki wachache waliufahamu na walishiriki kucheza mchezo huo.

## TZ Prisons yasuka upya mabeki wake

Na Shufaa Lyimo

KUELEKEA mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya KMC itakayochezwa Aprili 12, mwaka huu, benchi la ufundi la Tanzania Prisons linajipanga kuimarisha safu yake ya ulinzi ili kuhakikisha hawaruhusu nyavu zao kutikiswa.



Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Hamad Ally (pichani), aliliambia gazeti hili alibaini makosa machache katika safu hiyo kwenye michezo iliyopita, hivyo anarekebisha mapungufu hayo kwa lengo la kuhakikisha hayajirudii.

"Tunaendelea kujiimarisha kwa lengo la kupata pointi tatu katika mchezo wetu unaofuata, tunajua utakuwa na upinzani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na pande zote mbili," alisema Ally.

Aliongeza michezo ya kirafiki waliyoicheza imesaidia kuimarisha miili ya wachezaji wake na anaahidi watapata matokeo chanya na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kocha huyo alisema afya za wachezaji wake zinaendelea vizuri isipokuwa, Doto Shabani, ambaye ni majeruhi lakini anaamini hali yake itaimarika na kurejea kikosini hivi karibuni.

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL, BAYERN SOKONI

LIVERPOOL na Bayern Munich zinatathmini upya mipango yao baada ya Kocha, Xabi Alonso, kuamua kusalia Bayer Leverkusen, huku Barcelona wakitazamia kukamilisha dili la kumnunua Ruben Amorim kutoka Sporting Lisbon, kama mbadala wa Xavi anayeondoka. ***(Independent)***

### YAMWANIA KIMMICH

ARSENAL imewasiliana na Bayern Munich kuhusu uhamisho wa kiungo wao wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich, lakini wameambiwa mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 hautajadiliwa hadi msimu wa joto. ***(Football transfers)***

### AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL inaonekana iko katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi, mwenye umri wa miaka 25, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Bayern Munich. ***(Caught offside)***

### WIRTZ AOTA MBAWA

MANCHESTER City na Liverpool zinatarajia juhudi zake za kumsajili kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz, mwenye umri wa miaka 20, zitatatizwa na uamuzi wa Xabi Alonso kubakia katika klabu hiyo ya Bundesliga. ***(HITC)***

### UNITED KUBORESHA ULINZI

MANCHESTER United imewajumuisha wachezaji, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21 wa Everton, Aaron Anselmino (19) wa Boca Juniors na mchezaji wa kimataifa wa Senegal, Mikayil Faye, katika orodha yao ya kuimarisha safu ya ulinzi msimu huu. ***(Mail)***

### SANCHO ATAJWA UNITED

JADON Sancho, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Borussia Dortmund anaweza kupata fursa nyingine Manchester United ikiwa klabu hiyo itamteua Jason Wilcox wa Southampton kama Mkurugenzi wa Soka. Wilcox alifanya kazi na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 24 katika chuo cha soka cha Manchester City. ***(Manchester Evening News)***

### MCKENNA ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumteua Kocha wa Ipswich, Kieran McKenna, kama kocha wao mpya. Raia huyo wa Ireland Kaskazini mwenye umri wa miaka 37, aliwahi kufanya kazi katika timu hiyo kama msaidizi wa Jose Mourinho na Ole Gunnar Solskjaer. ***(Football Insider)***

### YORO ATAKIWA MADRID

REAL Madrid ingependa kumsajili beki wa kati wa Lille, Leny Yoro, mwenye umri wa miaka 18, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Manchester United, Liverpool na Chelsea - msimu huu baada ya Mfaransa huyo kuiambia klabu yake anataka changamoto mpya. ***(Athletic)***

### SPURS KUMUUZA EMERSON

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikalazimika kumuuza mlinzi wa Brazil, Emerson Royal, mwenye umri wa miaka 25, ili kusaidia fedha za uhamisho wao katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BARCA YAMTOLEA MACHO AMORIM

**LISBON,** Ureno

BARCELONA ipo katika nafasi nzuri ya kufikia makubaliano ya kumwajiri Kocha wa Sporting CP, Ruben Amorim, huku kukiwa na hofu Liverpool huenda ikaongeza nia yao ya kumtaka mwalimu huyo mwenye umri wa miaka 39, kwa mujibu wa ripoti.

**Kocha wa sasa wa Barca, Xavi atajiuzulu wadhifa wake mwishoni mwa msimu huu, na licha ya klabu hiyo kujaribu kumzuia, gwiji huyo wa Camp Nou hivi majuzi alisisitiza hajabadili uamuzi wake.**

Kutokana na hali hiyo, Barcelona wanasaka kocha mkuu mpya na kwa mujibu wa gazeti la The Independent, wanalenga kumtafuta Amorim.

Ripoti hiyo inadai Barcelona kwa muda mrefu inaonekana kupendezwa kumpata Amorim huku Liverpool na Bayern Munich, ambao pia wanahitaji makocha wapya kabla ya msimu ujao kuchukua nafasi za Jurgen Klopp na Thomas Tuchel, walikuwa na malengo ya kumchukua, Xabi Alonso wa Bayer Leverkusen.

Hata hivyo, huku Alonso hivi karibuni alithibitisha uamuzi wake wa kubakia msimu huu wa joto, mbio za kumwania Amorim zimepulizwa na Barcelona sasa wanasemekana wako mbioni kukamilisha dili kabla ya Liverpool au Bayern kujaribu kumpata.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, Makamu wa Rais wa Barcelona, Rafa Yuste, alikiri wazi ataendelea kujaribu kumshawishi Xavi kubaki, akipendekeza kwa sasa hakuna mpango wa kkutafuta mrithi kule Katalunya.

"Nitajaribu kumshawishi Xavi, lakini ni uamuzi ni wake kibinafsi," alisema Yuste.

"Bado kuna michezo ya ligi iliyobakia, Ligi ya Mabingwa Ulaya,... inabidi tumwache aifurahie. Natumaini na ninatamani aendelee kwa sababu tunazungumza juu ya mradi wa muda mrefu naye, sio msimu mmoja au miwili."

Kipengele cha juu cha kutolewa kwa Amorim, kinachoaminika kukaribia pauni milioni 13, kinaweza kuwa kikwazo kikubwa kwa Barcelona.

**●●● Kocha huyo pia anawindwa na Liverpool na Bayern Munich ili...**

# NEWCASTLE YAJITOSA TENA KWA RAMSDALE




**LONDON,** England

KLABU ya Newcastle United imerejea tena kutaka kumnunua mlinda mlango wa Arsenal, Aaron Ramsdale, ripoti mpya imedai.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amepoteza nafasi yake kwenye Uwanja wa Emirates kwa David Raya, ambaye yuko kwa mkopo kutoka Brentford, baada ya kukaa kwa misimu miwili kama kipa chaguo la kwanza wa klabu hiyo.

Chelsea imekuwa ikihusishwa kwa kiasi kikubwa na Ramsdale, ambaye alichukua jukumu muhimu katika harakati za Arsenal kuwania taji la Ligi Kuu England msimu uliopita, lakini 90min ilifichua mwishoni mwa Februari haiwezekani kuhamia Stamford Bridge katika hatua hii.

West Ham United pia imekuwa ikimfuatilia Ramsdale, ambaye anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake baada ya Euro 2024 msimu huu wa joto huku kukiwa na nia ya klabu nyingine kutoka Ulaya.

90min inaelewa Ramsdale, ambaye alijiunga na Arsenal mwaka 2021 kwa dili la pauni million 30, angependelea kubakia katika Ligi Kuu England, na Mail Sport iliripoti Newcastle inaweza kumpa njia nyingine kutoka London Kaskazini wakati wanataka kuimarisha kikosi chao.

Kocha, Eddie Howe, tayari amemsajili Ramsdale mara moja katika maisha yake ya soka, wakati akiwa Bournemouth, na inadaiwa mipango ya uhamisho ya Newcastle ni pamoja na kuleta mbadala wa makipa wawili, Martin Dubravka na Nick Pope.

Dubravka (35), kwa sasa anamiliki glavu huko Tyneside, huku Pope (32), akiendelea kupata nafuu kutokana na bega lake lililoteguka wakati wa mechi iliyofanyika Desemba mwaka jana dhidi ya Manchester United, lakini mkataba wa Mslovakia huyo una zaidi ya mwaka mmoja tu kukamilika.

Ramsdale ameichezea Arsenal mechi sita pekee za Ligi Kuu England msimu huu baada ya kuwasili kwa Raya.

# United pigo juu ya pigo

**MANCHESTER,** England

WALINZI wa Manchester United, Lisandro Martinez na Victor Lindelof wote watakuwa nje kwa angalau mwezi mmoja kutokana na majeraha ya misuli waliyoyapata siku za hivi karibuni.

Klabu hiyo ilithibitisha pigo hilo la majeruhi hao wawili katika taarifa yake jana usiku.

Lindelof alipata jeraha la misuli ya paja wakati wa sare ya 1-1 Jumamosi dhidi ya Brentford kwenye Ligi Kuu England, huku raia huyo wa Sweden akishindwa kumaliza pambano hilo Magharibi mwa London.

Martinez alichukua nafasi ya Lindelof baada ya dakika 69 za mchezo katika kurejea kwake kutoka kwa malalamiko ya awali ya goti. Lakini baada ya kucheza mechi yake ya kwanza tangu Februari, mwaka huu, alijikuta akijitonesha na hivyo kumlazimisha naye kuwa nje ya uwanja.

Beki huyo wa kati wa zamani wa Ajax aliumia katika mechi ya Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla Aprili mwaka jana, na kumlazimu kukosa mwisho wa msimu.


Baadaye alikuwa na wakati mbaya zaidi Agosti na akacheza mechi kadhaa kabla ya kuondolewa uwanjani hadi Januari. Alianza mara tatu tu kabla ya tatizo la goti la Februari.

Raphael Varane alitolewa wakati wa mapumziko dhidi ya Brentford kama tahadhari. Kutokuwepo kwake kwenye taarifa ya United kuhusu Martinez na Lindelof kunaweza kuwa dalili ya Mfaransa huyo kutokuwa na wasiwasi mkubwa. Jonny Evans pia alikosekana kwenye kikosi Jumamosi kutokana na jeraha.

Kwa jinsi mambo yalivyo, Harry Maguire ndiye beki pekee wa kati mwandamizi ambaye yuko fiti na anayepatikana kabla ya safari ya United kurejea London kumenyana na Chelsea leo.

Luke Shaw pia kwa sasa haypo kutokana na jeraha. Varane au Evans bado wanaweza kuwa katika kinyang'anyiro cha mchezo huo dhidi ya Chelsea.




# Ange: Spurs ipo njia sahihi

**LONDON,** England

ANGE Postecoglou alihisi sare ya 1-1 ya Tottenham Hotspur dhidi ya West Ham ilikuwa hatua nzuri licha ya kuangusha pointi zaidi katika mbio za nne bora kwenye Ligi Kuu England.

"Nilidhani kwa sehemu kubwa tulidhibiti mchezo vizuri," alisema bosi huyo wa Spurs.

"Ni timu kubwa yenye nguvu. Wanakaa ndani na kufanya iwe vigumu kwako. Lazima uwe mtulivu kiasi katika mbinu yako, lakini pia nidhamu kweli kwa sababu ni tishio kutoka kwa mashambulizi yao.

"Lakini ni binadamu, ni soka tu. Ningependa kuwa na kijiti cha furaha na kuziweka mahali ninapotaka, lakini haifanyi kazi hivyo.

"Wakati mwingine tunakuwa na wakati mwingi kuliko tunavyofikiria. Kulikuwa na nyakati ambapo mpira ulimwangazia kwenye boksi wakati tulipaswa kuwa katika maeneo hayo.

"Yote ni sehemu ya maendeleo. Ndio maana tuna makocha, ndiyo maana tunatengeneza mfumo. Sisi sio nakala iliyomalizika na tunajua hilo.

"Kulikuwa na yakutosha, naweza kusema kwamba ni timu ambayo bado inaelekea katika mwelekeo sahihi."

"Pengine ilikuwa haki mwishowe, tulifanya mambo mengi mazuri na tulionyesha ujasiri zaidi katika ulinzi," alisema bosi wa Hammers, David Moyes.

"Tulionekana tishio na ilibidi tufanye kazi nzuri kusimamisha timu nzuri sana ya Tottenham."

## HABARI MICHEZO

# TANESCO, Mwadui zatakata

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Tanesco, Mapinduzi, Rhino Rangers na Mwadui zimetinga hatua ya Nane Bora ya Ligi Daraja la Pili Ngazi ya Taifa 'First League' baada ya kumaliza zikiwa juu katika Kundi B.

Timu iliyoonekana kuwa tishio kwenye ligi hiyo, TRA FC, ambayo hivi karibuni iliondolewa katika michuano ya Kombe la FA na Simba, imeshindwa kupenya baada ya kumaliza ikiwa nafasi ya tano.

Mapinduzi FC imemaliza ikiwa ya kwanza kwenye kundi hilo, ikiwa na pointi 28 huku Rhino Rangers ikishika nafasi ya pili baada ya kujikusanyia pointi 27 na nafasi ya tatu imeshikiliwa na Tanesco yenye pointi 27, lakini ikiwa na idadi ndogo ya mabao ya kufunga.

Rhino Rangers imefunga mabao 34 wakati Tanesco imemaliza ligi ikiwa na mabao 29, huku na nafasi ya nne ikichukuliwa na timu isiyotegemewa ya Mwadui FC, iliyomaliza ikiwa na pointi 25.

Licha ya kumaliza ikiwa na pointi 25 kama Mwadui, kilichoiponza TRA, ambayo Februari 28, mwaka huu ilibugizwa mabao 6-0 na Simba katika Kombe la FA, ni idadi ndogo ya mabao ya kufunga, ikiwa imefunga 17 tu, huku wenzao wakipachika mabao 27.

Timu hizo nne, zitaungana na timu nyingine nne za juu zitakazomaliza katika Kundi A ili kucheza hatua inayofuata ya ligi hiyo.




Kiungo wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# SINGIDA BLACK STARS FC YAANIKA MALENGO YAKE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA kubadilishwa jina kutoka Ihefu FC na kuitwa Singida Black Stars, uongozi wa timu hiyo umesema sababu ya kufikia uamuzi huo imetokana na kuitaka klabu hiyo kuwa karibu na mashabiki wao wa mkoa wa Singida.

Mabosi wa timu hiyo pia wameweka wazi tayari wamekamilisha taratibu zote za usajili katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

**Mkurugenzi wa Utawala wa Singida Black Stars, Muhibu Kanu, alisema nia na malengo ya kubadilisha jina ni kuunganisha timu kwa wananchi wote wa Singida baada ya kuhamia mkoani humo tangu Februari, mwaka huu.**

"Nia na malengo ya kubadilisha jina ni kuiunganisha timu na wananchi wote wa Mkoa wa Singida, hasa ikizingatiwa kwa sasa imehamisha maskani yake kutoka ilipokuwa na kuja mkoani hapa.

Taratibu zote za usajili wa jina hilo zimeshamalika kwa kufuata mwongozo, kanuni na taratibu zote nchini, TFF na BMT na timu yetu hii tumelenga katika kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana wa nchi yetu ili kuinua maisha yao na kutimiza ndoto zao kupitia vipaji walivyonavyo," alisema Kanu.

Alisema ana imani kubwa wataendelea kushirikiana na wadau wote na kila mmoja kwa nafasi yake ili kuendeleza mpira wa miguu wa Tanzania.

Ihefu ilihamia mkoani humo, na kuamua kucheza mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa CCM Liti, Singida.

Na hii ilitokea baada ya baadhi ya wachezaji wa Singida Fountain Gate kuhamishwa katika klabu ya Ihefu kipindi cha usajili wa dirisha dogo.

Kwa sasa kikosi cha Singida Black Stars kiko Mwanza tayari kwa mechi ya Kombe la FA dhidi ya Tabora United itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

# *Simba na saa 120 'kuinyoa' Al Ahly*

INATOKA UKURASA 24

zitakazosaidia nyota wake kutumia kila nafasi watakayoipata dhidi ya Waarabu hao kuwa mabao.

"Tunahitaji kuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kupata matokeo ya mechi kubwa, ninaimani kubwa na wachezaji wangu na kile nilichowapa katika uwanja wa mazoezi ndani ya siku tano tunaweza kufanya vizuri ugenini," alisema kocha huyo.

Aliongeza haikuwa malengo yao kupoteza mchezo wa nyumbani lakini katika soka lolote linaweza kutokea, hivyo anaimani mechi ijayo watacheza kwa tahadhari kubwa ili kusonga mbele.

"Al Ahly ni timu kubwa, ipo wazi na ina wachezaji wenye uwezo mkubwa, nasi tunahitaji wachezaji wenye uwezo mkubwa katika kuendeleza ushindani. Makosa ambayo tumefanya, tumeyafanyia kazi na kwa sababu wachezaji wanafanya kazi kubwa kutimiza majukumu yao hilo linatupa nguvu kuamini tutafanya vizuri," alisema Benchikha.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' amesema wao ni wawindaji na wameenda Misri kushindana na kutafuta ushindi wa ugenini dhidi ya wenyeji wao Al Ahly.

"Tunaenda kukutana na timu tunayoijua, Kocha Benchikha amefanya kazi yake na viongozi tumemaliza majukumu yetu, katika kuhamasisha tunafanya vizuri katika mchezo wetu wa Ijumaa, Mwekezaji Mo Dewji ametoa ahadi ya kiasi kikubwa cha fedha (hakukitaja), kazi kubwa ipo kwa wachezaji wenyewe kupambana na kushinda mechi hii," Try Again alisema.

Katika hatua nyingine Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha timu hiyo kiliwasili Misri jana asubuhi na leo watafanya mazoezi ya mwisho kabla kuivaa Al Ahly hapo kesho.

Ahmed alisema kwa wachezaji waliopo katika mipango ya Benchikha wote wako fiti na hakuna mchezaji majerahi isipokuwa Aishi Manula ambaye alijitonesha kidonda alipokuwa katika majukumu ya Timu ya Taifa (Taifa Stars).

"Baada ya uchunguzi wa jopo la madaktari, Manula ameumia katika eneo la paja, ni pale alipoumia mara kwanza na kufanyiwa upasuaji, tumeshauriwa kipa huyo kukaa nje ya uwanja kwa muda wa wiki sita kwa ajili ya kupata matibabu na muda wa kupumzika ili kuja kuwa fiti," alisema Ahmed.

Kuelekea mechi ya kesho, Ahmed alisema wamefanya maandalizi ya kutosha na tayari Benchikha amerekebisha makosa aliyoyabaini ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya na kusonga mbele.

# Wachezaji Yanga wala kiapo Sauzi

INATOKA UKURASA 24

na imani wanakwenda kuandika historia.

"Kikosi kilikuwa kinafanya mazoezi siku zote tangu kilipowasili, lakini Alhamisi (leo), tutafanya mazoezi kwenye uwanja rasmi tutakaocheza, tuna imani tunakwenda kuandika historia siku ya Ijumaa," alisema meneja huyo.

Hersi Said, Rais wa Yanga, aliwashukuru maofisa wa ubalozi wa Tanzania walioko Afrika Kusini kwa mapokezi mazuri lakini akifafanua kuhusu basi walilotayarishiwa kuharibika wakati wanaelekea hotelini.

"Muda mfupi baada ya kuondoka gari letu lililobeba wachezaji ambapo kikanuni lilipaswa kuwa ni la wenyeji wetu lilipata hitilafu, lakini kutokana na maandalizi mazuri ya balozi na kikosi kazi chetu kilichotangulia, tulipata msaada wa haraka ambao haukuchukua hata dakika tano tukapata usafiri wa kutupeleka hotelini, baadaye tukawasiliana na wenzetu wa Mamelodi Sundowns ili watupatie basi lingine, lakini pia tumeshapata basi letu wenyewe lipo hapa hotelini, kwa maana hiyo tutakuwa nayo mawili, la wenyeji na tulilofafuta wenyewe," alisema Hersi.

Michezo
Alhamisi Aprili 4, 2024
Nipashe



Barca yamtolea macho Amorim UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayochezwa kesho jijini Cairo, Misri. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba na saa 120 'kuinyoa' Al Ahly

**Na Saada Akida**

## Benchikha afunguka 'wanajuana', Mo Dewji aongeza mzuka kuelekea...

WAKATI kikosi cha Simba kikiwasili salama Misri, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdelhak Benchikha, ameweka wazi ametumia siku tano 'kuisuka upya' safu yake ya ushambuliaji kwa ajili ya kuhakikisha inatumika vyema kila nafasi watakayoipata katika mechi ya marudiano dhidi ya Al Ahly itakayochezwa kesho jijini Cairo.

**Hatua hiyo imetokana na washambuliaji wa Simba kushindwa kutumia nafasi za kufunga walizotengeneza katika mechi ya mkondo wa kwanza iliyofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ambapo wenyeji walilala bao 1-0.**

Al Ahly itaikaribisha Simba katika mchezo wa marudiano wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakaocheza kesho kuanzia saa 5:00 usiku kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Cairo.

Licha ya Benchikha kuendelea na mambo ya kiufundi, pia Mwekezaji wa Simba, Mohammed Dewji (Mo Dewji), ametoa ahadi nono kwa wachezaji endapo watafanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo.

Tangu kumalizika kwa mchezo wa kwanza, Benchikha ametumia muda wote wa mazoezi kuwakumbusha safu yake ya ushambuliaji inayoongozwa na Fredy Michael, Pa Jobe Omar na Kibu Denis, kuongeza umakini.

Mbali washambuliaji hao lakini pia kiungo Clatous Chama, Fabrice Ngoma, Babacar Sarr, Saido Ntibazonkiza, Sadio Kanoute na Willy Essomba Onana, wamepewa maagizo maalumu yatakayowasaidia kupata matokeo chanya na vile vile kuwakumbusha kutoruhusu bao.

Benchikha amewasisitiza wachezaji wake kutokupoteza nafasi 'kizembe' kwa sababu mchezo huo ni wa maamuzi.

Kocha huyo alisema amefundisha mbinu mbalimbali

INAENDELEA UKURASA 23

# Wachezaji Yanga wala kiapo Sauzi

**Na Adam Fungamwango**

NYOTA wa Yanga wameahidi watacheza na kupambana 'Kufa na Kupona' ili kuhakikisha wanaiondoa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayoendelea.

Mamelodi Sundowns itaikaribisha Yanga katika mechi ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kuanzia saa 3:00 usiku kwenye Uwanja wa Loftus Versfeld, Pretoria.

Akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema yeye na wenzake wanafahamu jukumu linalowakabili la kuwapa furaha wanachama, mashabiki wa Yanga na Watanzania kwa ujumla, hivyo hawatofanya mzaha.

Mwamnyeto alisema wamejipanga kucheza katika kiwango cha juu ili kupata ushindi katika mechi hiyo ya ugenini.

"Wachezaji wote wapo katika morali ya juu, hata wale majeruhi wameshaanza mazoezi, kina Khalid Aucho wapo hapa, hali ya hewa ni nzuri, tukijiandaa vizuri tunaweza kubadilisha matokeo hapa hapa Afrika Kusini.

Na sisi kama wachezaji tumeshajipanga na kupeana majukumu tutafia uwanjani, kinachotupa jeuri pamoja na kupambana, kucheza kwa juhudi kubwa lakini nyuma yetu kuna sapoti kubwa ya mashabiki ambao wamesafiri kwa wingi kutoka nyumbani hadi huku na wengine tumewakuta huku huku," alisema nahodha huyo.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema kikosi chao leo kinatarajiwa kufanya mazoezi yake kwenye uwanja ambao itachezwa mechi hiyo, huku akiwa

INAENDELEA UKURASA 23



Rais wa Yanga, Hersi Said (kushoto), akimkabidhi kadi ya uanachama wa klabu hiyo, Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini, James Bwana, alipotembelea kambi ya timu hiyo iliyoko Pretoria tayari kwa ajili ya kuwakabili wenyeji Mamelodi Sundowns hapo kesho. **PICHA: YANGA SC**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >